epaper.ippmedia.com
www.ippmedia.com
0745 700710
LIKE & FOLLOW US
Alhamisi Septemba 26, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0581811
www.ippmedia.com
nipasheTZ nipasheTZ The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital



UKURASA 22

**'HATUJAJUA RODRI ATAKUWA NJE KWA MUDA GANI'**

SHAMBULIO RISASI 38

# Tundu Lissu kushtaki kampuni

• **Atoa** aliyonayo moyoni, ataja sababu kesi kufunguliwa Uingereza... *Endelea ukurasa 2*



Makamu Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) Bara, Tundu Lissu, akizungumza na waandishi wa habari, Dar es Salaam jana. **PICHA: IMANI NATHANIEL**





Mkazi wa mtaa wa Mwime-Makungu, kata ya Mwendakulima, wilayani Kahama, mkoani Shinyanga, Kumalija Budeba (kushoto), akijiandaa kulipakia jeneza kwenye gari la polisi baada ya kukamatwa akiwa ameliweka shambani kwake jana na kusababisha taharuki kwa wananchi. **Picha ndogo:** Budeba akiwa kwenye gari la polisi baada ya kukamatwa. **PICHA: SHABAN NJIA**

## Mganga azua taharuki kisa jeneza kukutwa shambani kwake

UKURASA 5

UKURASA WA 3

**JKT** yatangaza vijana kujiunga na mafunzo kujitolea, yaonya matapeli

UKURASA WA 4

**Mke** afichua siri mumewe alivyopigwa hadi umauti



UKURASA WA 11

**Simulizi** mwenyekiti wa wagumba alivyotaka kuiba mtoto, akashindwa



## Samia: Kataeni vishawishi kuvuruga amani ya nchi

UK. 2

**MICHEZO** **SIMBA SC, AZAM FC VITANI UGENINI** UK.24

**KATUNI** UK.6

# Samia ataka wanaoharibu amani wapuuzwe

Na Jenifer Gilla

RAIS Samia Suluhu Hassan amewasihi Watanzania kuwapuuzia wanaowashawishi kuharibu amani ya nchi kwa sababu zozote kwa kuwa kufanya hivyo kunarudisha nyuma maendeleo ya nchi.

Aliyasema hayo jana wakati akizungumza na wananchi wa Wilaya ya Mbinga akiwa katika siku ya tatu ya ziara yake mkoani Ruvuma na kuzindua jengo la Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga.

Pia alitembelea kituo cha ununuzi mahindi na soko la Jimbo la Mbinga Mjini, aliweka jiwe la msingi katika ujenzi wa Bandari ya Mbambabay na kufungua barabara ya Mbinga-Mbambabay yenye kilometa 60 iliyojengwa kwa kiwango cha lami.

Aliwasisitiza wananchi wa Mbinga wawapuuze wanaokwenda kuwashawishi kuharibu amani ya nchi kwa kuwa watu hao hawana nia njema, bali wanalenga kuharibu taswira ya nchi.

Alisema pamoja na changamoto mbalimbali zinazoikabili nchi, Tanzania ni sehemu salama ya kuishi akiita kuwa ni "pepo" kulinganisha na nchi nyingine.

"Ninataka kuwaambia kwamba wameishiwa, hawana pa kupenya, wameshaona mbele mambo magumu kwao, sasa la kufanya ni kuharibu amani na utulivu wa nchi yetu, ili wananchi waishi kwa shaka, mwone nchi yenu si njema, ndio lengo lao," alisema.

Rais alisema nchi inapokuwa na amani na utulivu, maendeleo hufanyika vizuri kwa sababu wananchi watakuwa na uhuru wa kufanya shughuli za maendeleo.

Akikagua jengo la Halmashauri ya Mbinga, Rais alisema kukamilika kwake kutarahisisha utoaji huduma kwa wananchi kwa kuwa maofisa kutoka idara mbalimbali watapatikana eneo moja.

Aliwaagiza viongozi wa wilaya kuwapa elimu wakulima juu ya madhara ya kuuza mazao yao kwa mawakala ikiwamo kulanguliwa, hivyo kukosa fedha za akiba na kujiinua kiuchumi.

Alisema mawakala hao wamekuwa wakinunua mahindi kwa wakulima kwa Sh. 300 kwa kilo kisha kwenda kuuza Sh. 700 bei ambayo mkulima anauza kwa Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA).

Rais pia alisema serikali inaendelea kutoa vibali vya kuongeza watumishi wa afya kadri bajeti inavyoruhusu ili kuziba pengo la uhitaji wa watumishi hao katika wilaya hiyo.

Pia alimwagiza Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, kupeleka wataalamu wa vizimba vya samaki katika wilaya hiyo na kuwafundisha wafanyabiashara teknolojia hiyo, ili serikali inapofunga shughuli za uvuvi kwenye maziwa kwa muda wasiathirike kiuchumi.

Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe aliwaahidi wakulima wa eneo hilo kuwa kuanzia mwakani, vituo vyote vya NFRA vitakuwa na mashine za kisasa za kusafisha mahindi, hivyo wakulima hawatosafisha kwa mikono kama wafanyavyo sasa.



Rais Dk. Samia Suluhu Hassan akivuta kitambaa kuashiria ufunguzi wa jengo la Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya Mbinga, mkoani Ruvuma jana. Kushoto ni Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mohamed Mchengerwa. **PICHA: IKULU**

# Lissu kushtaki kampuni ya simu

Na Romana Mallya

MAKAMU Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Tundu Lissu, amesema amewasiliana na mwanasheria wake kufungua kesi dhidi ya kampuni ya mawasiliano ya simu ambayo inadaiwa kuvujisha mawasiliano yake ya simu, hata kufanikisha shambulio la kupigwa risasi miaka saba iliyopita.

Ni hatua anayokusudia kuchukua baada ya gazeti la The Guardian la Uingereza juzi kuripoti kesi inayoendelea mahakamani nchini humo iliyofunguliwa na aliyekuwa Ofisa Usalama wa kampuni hiyo ya mawasiliano dhidi ya kampuni mama kwa kumwachisha kazi kutokana na anachodai kufanya uchunguzi dhidi ya wafanyakazi waliovujisha taarifa hizo.

Lissu ambaye alishambuliwa kwa risasi (inadaiwa risasi 38 zilielekezwa kwake akiwa katika gari lake) Septemba 7, 2017, kwenye eneo la nyumba za viongozi wa serikali jijini Dodoma, alitangaza hatua hiyo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari mkoani Dar es Salaam kuhusu kesi hiyo inayoendelea jijini London, Uingereza.

"Wamesema walikuwa wanatuma taarifa kwa njia ya WhatsApp, baadaye serikali ikawaambia wafute, itabidi wataalamu watuambie kama kuna uwezekano wa kurejesha taarifa zilizofutwa.

"Itabidi watuambie majina na itakayotuambia ni... (anataja jina la kampuni hiyo ya mawasiliano). Kampuni mama si wako Uingereza, tutaanza nao. Hatutakwenda kwenye mahakama za hapa. Tutakwenda Uingereza.

"Tukienda huko nimewaambia walianzishe, leo (jana) nimezungumza na Robert Amsterdam, nimemwambia una mamlaka kamili ya kulianzisha. Hatujazungumza madai ya fedha, ninafikiri yatakuwa mengi sana, hatujayajadili bado," alisema.

Lissu alisema tukio hilo katika tafsiri ya sheria, ni kitendo cha ugaidi kwa mujibu wa sheria za Tanzania; alipata ulemavu wa kudumu, hawezi kutembea sawasawa.

Alisema anatembea na risasi mgongoni na mwili umejaa vyuma kwenye goti mpaka kwenye nyonga, makovu ya risasi 16 zilizompata kati ya 38 na ya operesheni 25.

Lissu alisema watoto wake hawajarudi Tanzania miaka mitano na juzi walimpigia, wakimwambia wanapenda kurudi nyumbani, lakini walifikiria walivyomwona Nairobi, Kenya wanashindwa kurejea.

"Mke wangu ameshindwa kurudi nyumbani ameogopa. Mimi king'ang'anizi tu. Tunahitaji kuambiwa ukweli wote," alisema.

**WALIOMPIGA RISASI**

Lissu alidai vijana wawili waliompiga risasi wapo na wajulikana na kwamba muda ukifika atawataja, huku akitaja jina la kiongozi mmoja wa kisiasa kuwa ndiye aliongoza kikosi kumshambulia.

"Kwa sheria yetu, Katiba yetu, serikali haina rukhsa ya kupewa mawasiliano ya wateja, mtu ana haki ya faragha, polisi hawatakiwi kuchunguza mawasiliano ya raia.

"Kuanzia siku hiyo na miaka yote mpaka leo (jana), serikali siku zote imesema kwamba, hao walionishambulia katikati ya majengo ya serikali ni watu wasiojuliana.

"Serikali wakati ule kwa sababu sikuwapo nchini nikiwa nje kwa matibabu, walidai kwamba watalichunguza nitakaporudi Tanzania.

"Hawajachunguza mpaka sasa hivi, hata kuitwa polisi kuulizwa 'hebu tuambie umeona nini?' Niliona vijana wawili walionishambulia. Lakini kuitwa na polisi kusema niliona nini, hata hilo hawajawahi kufanya," alidai Lissu.

**FEDHA MATIBABU**

Lissu pia alisisitiza kauli yake ambayo huitoa kila mara akidai kwamba: "Sijawahi kulipwa hata senti moja ya matibabu. Sheria ya Uendeshaji Bunge ilitungwa mwaka 2008, inasema mbunge akiugua, serikali inawajibika kumpa matibabu ndani au nje ya nchi."

**RIPOTI YA THE GUARDIAN**

Kwa mujibu wa taarifa iliyochapishwa na gazeti The Guardian la Uingereza, aliyekuwa Ofisa Usalama wa kampuni hiyo ya mawasiliano ya simu, amefungua kesi nchini humo akidai kufukuzwa kazi bila haki baada ya kupinga hatua ya kutoa data za simu za mwanasiasa Tundu Lissu mwaka 2017 na kuvujishwa bila ridhaa yake.

Anadai kuwa akiwa mfanyakazi wa kampuni hiyo, alivutiwa na mazungumzo fulani yaliyofanyika kwenye mkutano wa mtandaoni na yeye akiwa mshiriki, na kwamba alishtuka kwamba kuna jambo linaendelea pasipo yeye kushirikishwa kama mkuu wa idara.

Anadai alianzisha uchunguzi binafsi na kubaini kulikuwa na mawasiliano yasiyo ya afya baina ya kampuni na idara fulani ya serikali, ambayo yalifanyika kupitia mtandao wa WhatsApp, kampuni hiyo ya simu ikivujisha taarifa binafsi za simu za Lissu.

"Uvujishaji ulianzia tarehe 22 Agosti 2017, lakini kuanzia Agosti 29, 2017 kukawa na uvujishaji mkubwa wa taarifa za Lissu mbashara (live tracking). Taarifa hizo zilihusu maeneo aliyopo Lissu, simu zinazoingia na kutoka zikisikilizwa na SMS (ujumbe) zake zikisomwa.

Anadai kuwa mawasiliano yale yalifutwa bila kuwapo nyaraka inayoelekeza vile na ndipo aliamua kuandika ripoti maalum juu ya alichobaini na kuwasilisha kwa wakuu wake akiwajulisha ana shaka kampuni yake ilishiriki kumuuza Lissu kwa watu waliokuwa na kiu na damu yake.

Badala ya suala hilo kufanyiwa kazi, Novemba mwaka huo alifutwa kazi kwa kigezo cha kupunguzwa kazini, lakini anaamini uchunguzi alioanzisha ulikuwa nyuma ya yote yaliyomtokea ndipo aliamua kwenda kudai haki mahakamani.

Nipashe ilimtafuta Msemaji Mkuu wa Serikali, Thobias Makoba, ambaye baada ya kuelezwa kuhusu suala hilo, alitaka atumiwe ujumbe wa maandishi. Alitumiwa, lakini hakujibu.

ATT

TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI ZA MADEREVA

KAMPUNI YA ATHWALS TRANSPORT AND TIMBER LIMITED, INAYO FURAHA KUTANGAZIA NAFASI YA KAZI YA UDEREVA , KWA WANANCHI WOTE WA KITANZANIA WENYE SIFA ZIFUATAZO:-

1. UWE UMEMALIZA DARASA LA SABA NA KUENDELEA
2. UWE UMEHUDHURIA KIKAMILIFU MAFUNZO YA UDEREVA NA KUHITIMU
3. UWE NA UMRI WA MIAKA 18 NA KUENDELEA
4. UWE NA UZOEFU WA KUENDESHA GARI NA TERA YAANI (TRUCK AND TRAILER)
5. UWE NA LESENI HAI YA UDEREVA
6. UWE NA UZOEFU WA MIAKA MITANO YA UENDESHAJI MAGARI MAKUBWA
7. UWE NA WADHAMINI WAWILI WANAOTAMBULIKA
8. UWE NA BARUA KUTOKA SERIKALI YA MTAA
9. UWE NA BARUA YA AFISA MTENDAJI KATA
10. AMBATANISHA NA PICHA TATU ZA PASSPORT SIZE

MAOMBI YOTE YAWASILISHWE AU YATUMWE KABLA YA TAREHE 7 OKTOBA 2024 YA KIWA NA VIAMBATANISHO VYOTE KWA

**MKURUGENZI**
**MAKAO MAKUU TABORA,**
**ATHWAL TRANSPORT AND TIMBER LTD**
**SLP 593, TABORA.**
**NAMBA ZA SIMU 0787225511, 0784621111, 0653842083, 0682882333**

# TLS, serikali kushirikiana uandishi mikataba

**Na Grace Gurisha**

CHAMA cha Wanasheria Tanganyika (TLS) na Chama cha Wanasheria wa Serikali (PBA), wamekubaliana kushirikiana katika maeneo saba yakiwamo kuishauri serikali, uandishi wa mikataba ya uwekezaji na kutoa fursa kwa mawakili wa ndani na si wa nje kuendesha kesi nchini.

Wakili Mkuu wa Serikali, Dk. Ally Possi, alisema jana jijini Dar es Salaam kuwa hati hiyo ya ushirikiano imeshaandaliwa na kwamba inapitia utaratibu wa kiserikali kabla ya kutiwa saini.

Alisema katika ushirikiano, suala la taaluma limepewa kipaumbele kwa sababu dunia imebadilika na kwamba kuna uwekezaji wa kimataifa unaofanyika kwa wawekezaji kuja Tanzania na Watanzania kwenda nje ya nchi kuwekeza.

"Iko fursa kwa wanasheria waliopo nchini kufanya kazi na wawekezaji badala ya wawekezaji kutumia wanasheria wa kigeni. Hili nalo tumelizingatia," alisema.

Dk. Possi alisema wanasheria Watanzania wapo, vyuo vya taaluma za sheria zinatoa wanasheria wa Tanzania, hivyo wanataka kukuza taaluma ili wanasheria watumie fursa hizo.

"Tutaendeleza maadili ya wanasheria kwani ni jambo endelevu kwa kuhakikisha wanafahamu masuala yanayohujumu uchumi wa nchi kama vile utakatishaji fedha," alisema.

Pia alisema wanasheria wanapaswa kujua uandishi wa mikataba na mambo yanayosaidia kufanyika kwa uhujumu uchumi ili kuepukana nayo na kusimamia maadili.

Alisema eneo lingine ambalo watashirikiana ni kufanya kazi kwa karibu na mahakama kwa kutatua migogoro nje ya mahakama ili kusaidia kupunguza mrundikano wa kesi mahakamani.

"Tanzania si kijiji kwani imejiunga na jumuiya mbalimbali za kimataifa, hivyo wanasheria waliopo waone fursa kwenye utengamano badala ya kuacha mawakili kutoka nje kufanya kazi hizo nchini," alisema.

Alisema mawakili binafsi wana mchango mkubwa katika maendeleo ya nchi, hivyo wataweka namna bora ya kuishauri serikali na mawakili wa serikali wawasaidie sekta binafsi kwenye masuala ya kuandika mikataba mbalimbali ya kodi, gesi, mafuta na uandishi wa sheria.

"Tunaamini TLS itawasaidia hata katika masuala ya bima ya afya, utetezi katika kesi za mirathi, ardhi na kazi hivyo, kusaidia wananchi kupata huduma bora," alisema.

Rais wa TLS, Boniface Mwabukusi, alisema mazungumzo yao yalilenga kutumia taaluma yao ya uwakili kuisaidia serikali kwa maslahi ya taifa husuan eneo la uwekezaji na kuhakikisha vyama hivyo vinakuwa na faida na tija.

"Tutashirikiana katika kuongeza uzoefu na kutekeleza majukumu yao kwa namna ambayo italeta tija kiuchumi, kijamii na kisiasa nchini," alisema Mwabukusi.

Pia alisema wamezungumza kuhusu kusaini hati ya makubaliano kati ya TLS na PBA namna ya kuhusiana, kufanya shughuli zetu na kushirikishana uzoefu katika shughuli mbalimbali.

Mwabukusi alisema watashirikiana namna ya kujenga na kusimamia sheria za ulinzi wa rasilimali na utukufu wa nchi katika kumiliki na kuendeleza rasilimali hizo.

Alisema sheria namba tano na sita zinawapa wajibu kuona tija ya kutungwa kwa sheria za ulinzi wa rasilimali hivyo kama wanasheria tunawajibu wa kulinda kwa maslahi ya taifa.

Mwabukusi alisema watashauri serikali kuhusu utatuzi wa migogoro ya uwekezaji badala ya kwenda kutatuliwa nje ya nchi, ifanyike nchini.

"Nia yetu uwapo wa TLS na PBA uwe daraja la kuhakikisha shughuli za uwekezaji zinanufaisha taifa, wananchi na wawekezaji na kulinda rasilimali hizo kwa maslahi ya kizazi kijacho," alisema.



Kaimu Mkuu wa Tawi la Utawala la Jeshi la Kujenga Taifa (JKT), Kanali Juma Mrai, akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dodoma jana, kuhusu nafasi za mafunzo kwa mujibu wa kujitolea. **PICHA: RENATHA MSUNGU**

# JKT yatangaza nafasi mafunzo ya kujitolea

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

JESHI la Kujenga Taifa (JKT), limetangaza nafasi za vijana kujiunga na mafunzo ya jeshi hilo kwa kujitolea kwa mwaka 2024 huku likitoa tahadhari ya matapeli wanaoomba fedha ili kuwatafutia nafasi jeshini.

Akizungumza na waandishi wa habari jana kwa niaba ya Mkuu wa JKT, Kaimu Mkuu wa Tawi la Utawala wa JKT, Kanali Juma Mrai, alisema utaratibu wa vijana kuomba na kuchaguliwa kujiunga na mafunzo hayo unaratibiwa na ofisi za wakuu wa mikoa na wilaya katika eneo analotoka mwombaji.

Alisema usaili wa vijana hao kujiunga na mafunzo hayo ya kujitolea umepangwa kuanzia Oktoba 2024 kwa mikoa yote ya Bara na visiwani na watakapochaguliwa watapoti kwenye kambi za jeshi kuanzia Novemba 1 na 3, 2024.

"Kumekuwa na wimbi la utapeli unaoendeshwa na baadhi ya watu ambao wakiwaomba fedha vijana wanaoomba nafasi hizo, naomba niwaambie nafasi hizi haziuzwi ni bure hivyo kila mmoja aombe sehemu husika zilizotolewa na JKT," alisema.

Aidha, alisema vijana hao ambao watachaguliwa kujiunga na mafunzo hayo, JKT haitoi ajira pia haihusiki kuwatafutia ajira katika asasi na vyombo mbalimbali vya ulinzi na usalama bali jeshi hilo hutoa mafunzo kwa ajili ya kuwaandaa vijana kwa ajili ya kujiajiri wao wenyewe.

Alibainisha sifa za waombaji wa nafasi hiyo kuwa ni vijana wa darasa la saba wanapaswa kuwa na umri kuanzia miaka 16 hadi 18 ambao wamemaliza elimu ya msingi kuanzia mwaka 2021, 2022 hadi 2023 wawe na cheti cha kumaliza elimu ya msingi.

Pia, alisema kwa vijana waliohitimu kidato cha nne kuanzia mwaka 2021, 2022 hadi 2023 wanapaswa kuwa na umri usiozidi miaka 20 na awe na ufaulu kuanzia daraja la kwanza hadi la nne na ufaulu uwe kuanzia alama 26 hadi 32.

Pia, alisema kwa waliohitimu kidato cha sita wawe na umri usiozidi miaka 22 ambao wamemaliza kuanzia mwaka 2021, 2022, 2023 na awe na cheti chenye ufaulu wa kuanzia daraja la kwanza hadi la nne.

"Vijana wa Stashahada umri usiwe zaidi ya miaka 25, wale wa shahada umri usiwe zaidi ya miaka 26 na wenye shahada ya uzamili umri usiwe zaidi ya miaka 27," alisema


## UBALOZI WA MAREKANI, DENMARK NA NORWAY DAR ES SALAAM

## MNADA WA HADHARA:

**UNIVERSAL AUCTION CENTRE** Kwa idhini waliyopewa na Ubalozi wa Marekani, Denmark na Norway watauza kwa mnada wa hadhara **Fanicha, Magari na Generator tarehe 28 Septemba, 2024 Jumamosi kuanzia saa 4:00 asubuhi.** Mnada utafanyika Golden Resort Sinza, Lion Street. Fanicha na Computer zitaanza kuuzwa kuanzia saa 4:00 asubuhi: Sofa sets, Chest drawer, Book case, Meza za ofisi, Viti, Makabati ya nguo,Steel file cabinet, Vitanda, Magodoro, Fridge double door Up Right Freezer, Washer, Dryer, Majiko ya Gas/Umeme, Meza za garden, Viti vya garden,Mashine za Photo copy Nashuatec MP6500, 5002, 2205 na Xerox 7970, Computer set, Printer HP Laser Jet, Flat TV, A/c split unit, na vingine **vingi.**

**Magari na Genereta yataanza kuuzwa kuanzia saa 6:00 mchana:**

| Idadi | Aina | Model | Mwaka | Ushuru |
|---|---|---|---|---|
| 2 | Toyota Land Cruiser V8 Station Wagon | 1VDO Diesel Engine | 2013 | Umelipwa |
| 1 | Jaguar Saloon Luxury | XF Petrol Engine | 2008 | Haujalipwa |
| 1 | Toyota Land Cruiser Prado S/ Wagon | 1KD Diesel Engine | 2002 | Umelipwa |
| 1 | Toyota Land Cruiser Station Wagon | 1KZ Diesel Engine | 1994 | Umelipwa |
| 2 | Generator KVA 500KVA – 3 Phase | Perkins Diesel Engine | - | Haujalipwa |
| 1 | Generator 150KVA 3 Phase | John Deer Diesel Engine | - | Haujalipwa |

Mali zote zinaweza kukaguliwa Golden Resort Sinza,Lion Street kuanzia tarehe 26 mpaka 27 Septemba 2024, kuanzia saa 4:00 asubuhi mpaka saa 11:00 jioni.

**MASHARTI YA MNADA.**

1. Mnunuzi wa Fanicha atatakiwa kulipa malipo yote kwa keshia (cashier). Na mnunuzi wa Gari au Generator atatakiwa kulipa 25% pale pale na salio lilipwe ndani ya siku 4 za kazi mwisho wa kulipa tarehe 3 Oktoba, 2024 Saa 10:00 jioni. Ukishindwa kulipa kwa muda huo Gari au Genereta litauzwa kwa mshindi mwingine aliyefata na dhamana haitarudishwa.
2. Malipo kwa njia ya VISA na Master cards za CRDB na NBC yanakubalika.
3. Mali zote zitauzwa kama zilivyo bila dhamana.
4. Mnunuzi atawajibika kulipa ushuru na kodi zingine zote.
5. Mali yote iliyouzwa itatakiwa kuondolewa baada ya kulipa malipo yote pamoja na kodi
6. Kila mtu atatakiwa lazima kuwa na bid namba itakayopatikana getini na kuvaa barakoa.

**UNIVERSAL AUCTION CENTRE DAR ES SALAAM**
**PLOT NO: 5 "E" LION STREET SINZA**
**CELL NO: 0754 284 926** **E-mail: universalauction@hotmail.com**
**Insta: universalauctioncentre**

# Familia yafichua siri ndugu yao alivyopigwa hadi kufariki dunia

**Na Mwandishi Wetu,** ARUSHA

MAPYA yameibuka kuhusiana na kifo cha utata cha mfanyabiashara wa vyuma chakavu katika Kata ya Muerieti, Johnson Josephat, maarufu KAMA Sonii (39), anayedaiwa kufariki dunia baada ya kutoroshwa na kundi la watu waliokuwa wakipinga kukamatwa kwake baada ya kufungwa pingu mkono mmoja na Polisi.

Sonii, Mkazi wa Unga Limited jijini Arusha, alifariki dunia Septemba 23, mwaka huu, katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Arusha ya Mount Meru, wakati akipatiwa matibabu.

Akizungumzia tukio hilo lililoibua simanzi katika viunga vya jiji la Arusha, mke wa marehemu, Nasra Bakari, alisema mtoto wake alishuhudia tukio zima la baba yake kupigwa na askari polisi, na ndiye aliyekwenda akikimbia kumpa taarifa kwamba baba anapigwa.

"Nilitoka nje nikakuta wamemnyonga, kichwa kwenye mapaja, mkono nyuma. Walikuwa askari wawili, nikaingia hapo tukawa tunaparangana nao, tukahangaika nao, (marehemu) akachomoka akakimbia akaanguka, akaangukia kichwa.

"Baada ya kuanguka, wakatokea tena watu wengine maana kulikuwa hakuna wanaume, ni wanawake tu. Wakaendelea kupambana na wale askari wawili, yule baba akakimbia tena akaingia uchochoroni na wale askari tena wakamkimbiza wakamfuata huko uchochoroni.

"Huko uchochoroni kuna mabanzi, hiyo nyumba ina mabanzi, wakawa wamemchukua wamemwingiza kwenye hayo mabanzi, kichwa kikawa kimeingia huko, ukabaki mwili.

Hatukufika pale kwa sababu kulikuwa hakuna wanaume, tulikuwa tunaparangana na wale maaskari wakamkanyaga kichwa," alisema.

Kutokana na vuta ni kuvute hiyo, mke wa marehemu alisema bahati nzuri, baada ya wanawake wale kuona hali ilivyo, walikwenda kuita wanaume ambao walifika sehemu walipokuwa wameingiza kichwa chake kwenye mabanzi na kubaini kwamba ameshapoteza fahamu, ndipo wakampeleka hospitalini.

Nasra, kupitia video iliyosambaa mtandaoni, alifafanua zaidi mkasa huo ulivyokuwa akisema: "Sasa wenyewe wanavyojielezea wanasema kuna mtu alikamatwa yuko huko Central (Kituo Kikuu cha Polisi Arusha), aliiba kompresa akamuuzia yeye (marehemu). Sasa tulivyofika eneo la tukio, nikawaambia haya masuala si ya kuongea kama mnaye.

"Wakasema hatutaki kuongea tunataka tumpeleke polisi. Baada ya tukio, walikuja askari wengine, ndiyo wakampeleka Mount Meru, tangu hapo alikuwa ameshafariki (dunia).

"Maana yake walihangaika kufungua ile pingu tangu tukiwa huku nyumbani. Tulipofika Mount Meru wengine wakarudi Central kutafuta funguo nyingine wakafungua ile pingu, ndio wakamwingiza hospitalini. Alikuwa ameshafariki tangu akiwa nyumbani."

Kupitia taarifa kwa vyombo vya habari iliyotolewa Septemba 24 na Kamanda wa Polisi, Kamishna Mwandamizi Msaidizi wa Polisi (SACP) Justine Masejo, tukio hilo lilitokea Septemba 23, saa 11:30 jioni.

Taarifa hiyo ilisema askari polisi ambaye hajatajwa jina wala namba yake ya kijeshi, alifika maeneo ya Unga Limited kwa ajili ya kumkamata mtu huyo kuhusiana na tukio za kuvunja stoo na kuiba.

Iliongeza taarifa hiyo kwamba wakati wa ukamataji, askari alifanikiwa kumvisha pingu mkono mmoja, ndipo lilipojitokeza kundi la watu na kumshambulia askari kumkamata mtu huyo na kumtorosha kwa kutumia pikipiki.

Kwa mujibu wa SACP Masejo, taarifa za awali zinaonyesha kuwa katika harakati za kumtorosha mtu huyo, alianguka na baadaye ndugu walimfikisha hospitalini.

Kamanda Masejo alisema uchunguzi wa tukio hilo unaendelea ili kubaini kilichosababisha kifo na wote waliohusika watachukuliwa hatua za kisheria.

**"Hata kwenye suala la kupanda madaraja Rais Samia ametuona sana sisi walimu, hata mishahara yetu mwalimu mwenye cheti ailingani na kada nyingine," alisema Ambindile.**

# Mwinyi ataka ushirikiano wizara za mazingira

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amezitaka wizara zenye dhamana ya mazingira za Muungano na Zanzibar, kufanya kazi kwa pamoja ili kuzipatia ufumbuzi changamoto za kimazingira na mabadiliko ya tabianchi zinazoibuka maeneo mbalimbali ya nchi.

Wizara hiyo ni Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) na Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar

Dk. Mwinyi aliyasema hayo jana Ikulu, Zanzibar alipokutana na kuzungumza na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Dk. Ashatu Kijaji, aliyeambatana na timu ya watendaji wakuu wa wizara hiyo, waliofika kujitambulisha.

Taarifa iliyotolewa na Idara ya Mawasiliano Ikulu, Zanzibar, ilisema Dk. Mwinyi alisema ni vyema wizara hizo mbili zikaweka mkazo katika kuzipitia sera, kanuni, miongozo, mipango na mikakati ya kudhibiti athari za mazingira na mabadiliko ya tabianchi kwa pamoja ili kubadilishana uzoefu na kuibua utatuzi wa masuala hayo.

Alisema uvamizi wa majichumvi kwenye maeneo ya kilimo, visima na makazi ya wananchi, mporomoko wa fukwe za bahari na ukosefu wa mvua na mvua zisizotarajiwa bado ni matatizo yanayoathiri kwa kiasi kikubwa.

Rais Mwinyi aliwataka watendaji wa wizara hizo kutumia makongamano na mikutano ya kimataifa ya kimazingira kuziwasilisha changamoto hizo zinazoikabili nchi ili kupata ufadhili na rasilimali za kukabiliana nazo.

Aidha, aliwasisitiza kuwa na mipango shirikishi kuanzia ngazi za chini kwa jamii ili nayo itoe mchango wake.

Dk. Mwinyi pia alisema Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeendelea kuchukua hatua mbalimbali za kuzuia athari za mazingira zisiendelee kuathiri maisha ya watu.

Kuhusu Muungano, Rais Mwinyi aliridhia ombi la Waziri Kijaji la kutaka siku tatu kila mwezi kwa watendaji wa wizara hizo mbili kukutana Zanzibar na kuwa na mikutano na wananchi kutoa maoni yao juu ya changamoto za Muungano.

Kuhusu biashara ya kaboni (gesi ukaa), Dk. Mwinyi aliwataka watendaji hao kushirikiana kwa pamoja, kujengeana uwezo na kuwatafuta wataalamu kwani biashara hiyo ni mpya ulimwenguni.

Pia alisisitiza suala la uratibu wa shughuli za Muungano kwa kuwa sekta zote wanazozisimamia zinahitaji ushirikiano wa karibu ili kuleta ufanisi.

Naye Waziri Kijaji alisema tayari wizara hiyo imeandaa timu ya wataalamu na imeanza utafiti na kuandika miradi kwa lengo la kuiwasilisha kwa wafadhili ili kupata fedha zitakazoendesha miradi ya kimazingira.

Alibainisha kuwa uharibifu wa mazingira ni mkubwa hasa katika fukwe unaosababishwa na mmong'onyoko na uvamizi wa maji chumvi katika maeneo ya kilimo, hivyo juhudi za pamoja zinahitajika kukabiliana na hali hiyo.

Waziri Kijaji alifika ikulu kujitambulisha baada ya kuteuliwa na Rais Samia Suluhu Hassan, Julai 3, mwaka huu, akitokea Wizara ya Viwanda na Biashara.


MuCoBa Bank PLC
"Kwa Maendeleo Yako"
P. O. Box 147, Tel. 026-2772165, Fax 026-2772075, Mafinga, Tanzania.
E-Mail: mucoba@mucobatz.com

**TAARIFA YA MKUTANO DHARURA WA WANAHISA WA BENKI YA MUCOBA**

Taarifa inatolewa kwa wanahisa kwamba, kutakuwa na mkutano wa dharura wa Wanahisa utafanyika siku ya Jumamosi tarehe 5 mwezi wa Oktoba 2024 katika ukumbi wa MAM –uliopo Mafinga Mjini kuanzia saa tatu kamili asubuhi.

**AJENDA YA MKUTANO ITAKUA KAMA IFUATAVYO:**

1. Kufungua Mkutano
2. Kuthibitisha Akidi ya Wajumbe
3. Kuridhia ajenda ya Mkutano
4. Kujadili maboresho ya makubaliano ya kimkakati baina ya Benki ya watu wa Zanzibar (PBZ) na Benki ya MUCOBA
5. Kufunga Mkutano.

Notisi hii imetolewa leo tarehe 26/09/ 2024

**MAMBO YA KUZINGATIA**

1. Mwanahisa anayetarajia kuhudhuria Mkutano huu atatakiwa kufanya hivyo kwa gharama zake mwenyewe.
2. Iwapo Mwanahisa anayeruhusiwa kuhudhuria Mkutano na kupiga kura, atashindwa kwa sababu zozote zile kuhudhuria Mkutano, ataruhusiwa kuchagua Mwakilishi kuhudhuria na kupiga kura kwa niaba yake kwa kufuata na kuzingatia taratibu na sheria za Kampuni.
3. Nakala za Makabrasha ya Mkutano zitapatikana pia kwenye ofisi yetu kuu iliyopo Mafinga- Iringa.

**KWA AGIZO LA BODI YA WAKURUGENZI**
**DENIS RWEYENDERA**
**KATIBU - BODI YA WAKURUGENZI**

## Mwalimu mbaroni tuhuma za kumuua mwanafunzi

**Na Vitus Audax**

ADRIAN Tinchwa (36), Mwalimu wa Shule ya Msingi Igurwa na Mkazi wa Kanoni, wilayani Karagwe, mkoani Kagera anashikiliwa na Jeshi la Polisi mkoani humo kwa tuhuma za kumshambulia na kumsababishia kifo Mwanafunzi Phares Buberwa, akimtuhumu kumwibia simu.

Mwanafunzi huyo aliyekuwa akisoma kidato cha tatu katika Shule ya Sekondari Igurwa, anadaiwa kukutwa akitoka ndani kwa mwalimu huyo (mtuhumiwa) ambaye alikuta kufuli la nyumba limevunjwa.

Akitoa taarifa ya kukamatwa kwa mwalimu huyo juzi, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kagera, Blasius Chatanda alisema mtumishi huyo wa umma anadaiwa kumshambulia mwanafunzi huyo kwa kumpiga ngumi kwenye paji la uso kisha kutumia nondo kumpiga nayo miguuni na mikononi akimtuhumu kumwibia simu yake.

Kamanda Chatanda alisema tukio hilo lilitokea Septemba 18, 2024, saa nane mchana katika Kijiji cha Kanoni, wilayani Karagwe.

"Awali tarehe hiyo hiyo majira ya saa tatu asubuhi, inadaiwa kuwa mtuhumiwa huyo alifika nyumbani kwake na kukuta kufuli la mlango wa nyumba yake limevunjwa na alipotaka kuingia ndani alikutana na Phares Buberwa, mlangoni akijaribu kukimbia," alisema Chatanda.

Alisema kuwa baada ya hapo alimkamata na kuanza kumshambulia hadi kumsababishia majeraha makubwa mwilini mwake na baadaye kumpeleka hadi nyumbani kwa wazazi wake na kumkabidhi kisha wazazi wake walimpeleka katika Kituo cha Afya cha Rwambaizi kwa ajili ya kupata matibabu.

"Phares alifariki dunia kituoni huko wakati akipatiwa matibabu na chanzo cha tukio hili ni mtuhumiwa kujichukulia sheria mkononi na kutoa adhabu iliyopitiliza kwa marehemu huyo hadi kufikia hatua ya kukimbizwa kituo cha afya," alisema Kamanda Chatanda. Alisema jeshi hilo linaendelea na uchunguzi zaidi kuhusiana na tukio hilo na mtuhumiwa atafikishwa mahakamani mara tu baada ya taratibu zote kukamilika.

"Wito wangu kwa wananchi ni kuacha tabia ya kujichukulia sheria mkononi badala yake wafuate taratibu zote za kisheria pindi wanapokamata wahalifu kwani hatutasita kuwachukulia hatua wote watakaoshindwa kufuata sheria kwani hakuna aliye juu ya sheria," alisema Kamanda Chatanda.

# Jeneza lakutwa shambani, ladaiwa kufichwa na mganga wa kienyeji

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WAKAZI wa mtaa wa Mwime-Makungu, kata ya Mwendakulima, Halmashauri ya Manispaa ya Kahama, mkoani Shinyanga, wamepatwa na taharuki baada ya Kumalija Budeba (55) anayedaiwa kuwa ni mganga wa jadi kukutwa akiwaameficha jeneza tupu kwenye kichaka kilichoko karibu na shamba lake huku akiwazuia watu kupita karibu na eneo hilo.

Tukio hilo lilitokea jana baada ya vijana waliokuwa wakichunga mifugo kuona jeneza hilo kisha kutoa taarifa kwa uongozi wa mtaa; nao ulitoa taarifa polisi waliofika na kumchukua Budeba kwa hatua za kisheria.

Kiongozi wa walinzi wa jadi katika mtaa huo, Someke John alisema kuwa baada ya kufika eneo la tukio walilazimika kulifungua ili kujiridhisha kama kulikuwa na mwili wa binadamu kutokana na taarifa awali kudai kuwamo maiti ndani ya jeneza hilo, lakini lilikuwa tupu.

Alisema kuwa walipomhoji alikiri kulifahamu na kudai kuwa lilikuwa linatumiwa na msanii (jina lake tunalo) aliyefika nyumbani kwake kumfundisha kijana wake namna ya kuimba nyimbo za asilia kwa ajili ya kutumbuiza kwenye matamasha ambayo wamekuwa wanafanya na aliweka shambani mwezi Julai mwaka huu ili watu wasipite.

Mkazi wa Mtaa wa Mwime, Matha Mihambo, alisema jeneza hilo limewashangaza kwani katika uwasilishaji sanaa ya muziki wa nyimbo za asili, hakuna kipengele cha kutumia jeneza, hivyo Kumalija alipaswa kuwa na kibali cha kulitumia na kuliweka nyumbani ili kutoibua maswali kwa wananchi.

Alisema hawajawahi kuona sanaa ya nyimbo za asili za jamii ya kisukuma ikitumia jeneza katika matamasha ya muziki na badala yake wamezoea kuona ikitumia nyoka wakubwa na kuomba serikali kumbana zaidi ili kujua alikuwa na maana gani kuwa na jeneza hilo shambani.

Awali akieleza kuwapo jeneza hilo shambani kwake, Kumalija Budeba alikiri kufahamu kuwapo jeneza hilo, akidai walikuwa wanalitumia kwenye matamasha ya muziki wa asili tangu mwaka jana.

"Msanii wangu ... (anataja jina la msaani wa Kanda ya Ziwa) aliliacha hapa baada ya kumaliza matamasha ya ngoma za asili. Nimeshangaa kuona kundi la watu wakivamia nyumba yangu, wakihoji juu ya uhalali wake na nina kibali kutoka Manispaa ya Kahama," alidai Budeba.

Hata hivyo, Ofisa Utamaduni wa Halmashauri ya Manispaa ya Kahama, Felix Ntibabara, alisema hawajawahi kutoa kibali cha matumizi ya jeneza kwa ajili ya shughuli za sanaa za asili na katika uwasilishaji maudhui ya nyimbo za asili ni kosa kutumia aina hiyo ya sanaa kwani ni kuwatisha wananchi badala ya kuwaburudisha.

Kaimu Kamanda wa Polisi mkoani Shinyanga, ACP Kennedy Mgani alithibitisha kukamatwa kwa Budeba na kuwa uchunguzi wa tukio hilo unaendelea ili kujua chanzo cha jeneza hilo kuwa shambani kwa mganga huyo.

Kamanda Mgani alisema jeneza hilo hivi sasa liko Kituo cha Polisi Kahama na ikibainika alikuwa analitumia kwenye vitendo viovu, atawajibishwa kwa mujibu wa sheria.



Mjumbe wa Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi, Dk. Zakia Mohamed Abubakar (katikati), akishuhudia wakati Mkuu wa Mkoa wa Singida, Halima Dendego (kulia), akichukuliwa taarifa zake na Mwandishi Msaidizi, Failuna Bira katika Kituo cha Chuo cha Ufundi na Marekebisho kwa watu wenye ulemavu Sabasaba, Kata ya Utemini, Manispaa ya Singida, jana. Wananchi wa mkoani Singida wameanza kujiandikisha na kuboresha taarifa zao katika Daftari la Kudumu la Wapigakura kuanzia jana hadi Oktoba 1, mwaka huu. **PICHA: INEC**

# Real Hope yaungana na wazazi mapambano ukatili kwa watoto

**Na Agustino Kihombo,** IRINGA

BAADHI ya wazazi na walezi mkoani Iringa wameanza kuweka mikakati ya kukabiliana na matukio ya ukatili wa kijinsia kwa watoto hasa ubakaji na ulawiti kwa kuweka ulinzi shirikishi kwenye mitaa na vijiji.

Wakati mikakati hiyo ya ulinzi shirikishi ikiwekwa, uongozi wa mkoa umewataka wazazi na walezi kuwajenga kiimani watoto ili kujenga taifa lenye hofu ya Mungu ambalo litakuwa mstari wa mbele kukemea matukio ya ukatili.

Akizungumza katika mahafali ya darasa la saba katika Shule ya Real Hope iliyoko mjini Mafinga, Mkuu wa Mkoa wa Iringa, Peter Serukamba, alisema katika siku za karibuni, matukio ya ukatili kama ulawiti na ubakaji yameendelea kuchukua sura tofauti baada ya ndugu wa karibu, ambao wasingedhaniwa kufanya vitendo hivyo, wanahusishwa kushiriki.

Serukamba alisema wengine wanawatisha watoto baada ya kuwafanyia vitendo hivyo na kusababisha kushindwa kutoa taarifa kwa wazazi wao.

"Kuna mjomba kaja kutoka porini huko na tabia zake anafika nyumbani wazazi mnamwambia alale na watoto. Matokeo yake anawafanyia vitu vibaya watoto anakimbia humwoni tena.

"Ushauri wangu wakeni mbali watoto wenu na wajomba hawaaminiki sasa. Watawaharibu watoto wenu na mbaya zaidi hata mkiambiwa mjomba ndiye kafanya, mnawakingia vifua na mnataka kuyamaliza kifamilia na mwisho wa siku anayeumia ni mtoto, hatua za kisheria hazichukuliwi," alisema.

Kuhusu elimu, Serukamba aliwataka wazazi kuwekeza zaidi kwa kuwaendeleza watoto wao katika ngazi inayofuata kwa kuwa ndio msingi wa kuwaandaa kuwa watu bora na viongozi wazuri ndani ya serikali na ndani ya nchi.

"Endelezeni watoto hawa bado ni wadogo, tusiwaache mtaani au tukawaacha walelewe na watu wasio wema. Watoto hawa ndio viongozi wetu wa kesho na tusiwabague, awe wa kike au wa kiume wote ni sawa na wapate elimu stahiki," alisema.

Dickson Mwipopo, ni Mkurugenzi Mtendaji wa shule za Real Hope, alisema miongoni mwa mambo wanayoyapa kipaumbele katika utoaji wa elimu ni maadili na malezi.

Alisema kwa kuzingatia utamaduni wa kitanzania, shule imetenga maeneo kwa ajili ya stadi za maisha kama mashamba ili kuwaandaa watoto kukabiliana na changamoto za maisha pindi wanapohitimu masomo huku wakishirikiana na wazazi katika kuwaandaa kuwa watu bora katika jamii.

"Tumekuwa na vikao vya mara kwa mara baina ya bodi ya shule na wazazi. Miongoni mwa malengo ya vikao hivyo ni kujadili namna bora ya kuboresha malezi kwa watoto pindi wanapokuwa nyumbani na shuleni.

Pia tumezungumza namna bora ya kuwalinda watoto dhidi ya vitendo vya ukatili, hivyo tumefanikiwa sana kutokomeza vitendo hivyo vinavyokatisha ndoto za watoto," alisema.

Alisema jitihada zingine wanazozifanya ni kuwajengea uwezo wanafunzi kujitambua kwa kuanzisha klabu za mapambano dhidi ya ukatili wa kijinsia kwa kuwafundisha kuwa na ujasiri vinapotokea vitendo ili watoe taarifa kwa walimu ili hatua za kisheria zichukuliwe jambo ambalo alisema limekuwa na matokeo chanya.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Huduma bora ziendane na mpango kukuza sekta utalii

**UTALII** ni moja ya sekta muhimu nchini katika kuchangia pato la taifa na kuzalisha ajira za moja kwa moja na zisizo za moja kwa moja nchini. Kwa mujibu wa takwimu za sasa, sekta hiyo inachangia asilimia 17 ya pato la taifa, hali inayodhihirisha kwamba ni eneo muhimu linalopaswa kupewa kipaumbele cha kipekee.

Ukuaji wa sekta hiyo, kwa kiwango kikubwa unatokana na vivutio mbalimbali zikiwamo hifadhi za taifa kama vile Mikumi, Ngorongoro, Serengeti, Manyara, Tarangire, Udzungwa na Ruaha. Hifadhi hizo zina vivutio vingi kama vile wanyamapori wakiwamo simba, tembo, faru, twiga na nyati ambao huwafanya watalii wa ndani na nje kutembelea maeneo hayo na kujionea rasilimali hizo asilia.

Kwa takribani miaka mitatu na nusu tangu Rais Samia Suluhu Hassan alipoingia madarakani, kumekuwa na ongezeko kubwa la watalii wanaofika katika hifadhi hizo, hivyo kuiwezesha nchi kupata fedha za kigeni kwa kutembelea hifadhi, kulala katika hoteli na kununua bidhaa mbalimbali za asili za Tanzania.

Kwa mujibu wa takwimu za Wizara ya Maliasili na Utalii, katika mwaka wa fedha wa 2023/24, idadi ya watalii kutoka nje ya nchi, waliongezeka hadi kufikia 1,808,205 kutoka watalii 922,692 mwaka 2021. Ongezeko hilo kwa kiasi kikubwa lilitokana na kutangazwa kwa vivutio vya utalii nchini kulikochagizwa na filamu ya 'The Royal Tour' iliyochezwa na Rais Samia.

Filamu hiyo iliitangaza Tanzania kwa kiwango kikubwa, hivyo kufahamika kimataifa kuwa ina vivutio vingi na kuwafanya watalii kuiona kuwa sehemu muhimu ya kutembelea na kushangaa maajabu yaliyomo ndani yake hasa wanyamapori waliomo katika hifadhi za taifa.

Kutokana na kasi ya kuitangaza nchi nje ya mipaka na duniani kwa ujumla, Waziri wa Maliasili na Utalii, Pindi Chana, mapema wiki hii alisema lengo la serikali ni kufanya jitihada za kuboresha utalii ili kuhakikisha watalii wanaoingia nchini wanafikia milioni tano ifikapo mwaka 2025. Iwapo azma hiyo itafikiwa, ni wazi kwamba serikali itapata fedha nyingi za kigeni kupitia sekta hiyo na hatimaye kuchangia zaidi katika pato la taifa.


Malengo yaliyowekwa kwa kufikisha watalii milioni tano ndani ya muda mmoja ni makubwa, hivyo yanahitaji juhudi za pamoja kati ya serikali na wadau, kwa mantiki hiyo, nguvu zaidi zinatakiwa kuendelea kutangaza vivutio vya utalii vilivyoko nchini ili kuwafanya watalii kuja kwa wingi na kufikia idadi iliyokusudiwa.

Sambamba na hayo, miundombinu kuelekea kwenye hifadhi za taifa kama vile barabara na viwanja vya ndege vinapaswa kuimarishwa ili kuwawezesha watalii kufika kwa urahisi. Viongozi wa serikali walioko katika mikoa yenye vivutio hivyo, wanapaswa kuweka suala la utalii ajenda namba moja katika shughuli zao za kila siku.

Kama alivyosema Rais Samia wakati akiwaapisha viongozi, alimwelekeza Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Paul Makonda, kusimamia suala la utalii kutokana na mkoa huo kuwa kitovu cha sekta hiyo. Kwa mpango wa kuongeza idadi ya watalii, Makonda alikuwa kiwakilishi cha viongozi ambao mikoa yao ina vivutio hivyo, hivyo nao wanapaswa kuzingatia maelekezo hayo.

Licha ya wajibu huo wa viongozi, sekta binafsi, hususan wamiliki wa hoteli na migahawa ya chakula pamoja na huduma zinazohusiana na utalii moja kwa moja, wanapaswa kuboresha huduma zao ili kuhakikisha watalii wanapofika, wanapata huduma za viwango vya juu na hatimaye wanaporejea kwao wanakuwa mabalozi wazuri wa kuitangaza Tanzania na vivutio vyake.

Kwa mikakati ya pamoja na ushirikiano baina ya sekta binafsi na ya umma, azma ya kuifanya Tanzania kuwa kitovu cha utalii itaongezeka na hatimaye sekta hiyo kuchangia ukuaji wa uchumi na pato la taifa maradufu au zaidi kulinganisha na hali ilivyo sasa.




Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com

## Muungwana Lazima Nilonge



Na Yasmine Protace

# Mvua 'kiduchu' sokoni Mabibo, maisha yanarudi ukodishaji mabuti ya tope

**MVUA** ni mtaji mkubwa kwa mazingira, ingawaje zinapozidi nazo zinahamia upande wa athari katika maisha ya mazingira kijamii.

Hadi sasa mvua zinazonyesha kiasi katika maeneo mbalimbali ya mkoa wa Dar es Salaam, zimekuwa zikigusa moja kwa moja mustakabali wa biashara na wafanyabiashara katika masoko, ambayo miundombinu yake haipo vizuri.

Katika soko la Mabibo, Dar es Salaam ambako huingiza bidhaa kutoka mikoa mingine mbalimbali nchini na wanaofanya baadhi ya aina ya uchuuzi, wanakimbilia huko kupata bidhaa, mvua zinaponyesha sokoni humo, baadhi ya maeneo huwa na matope mengi sana.

Matope hayo katika soko hilo, yanawaibua kinamama nao wanatumia fursa hiyo kukodisha mabuti kwa watu wahitaji, kwa ya shilingi 1000.

Zuwena Juma, mkazi wa Mabibo, Dar es Salaam, anasema kuwa mvua zinaponyesha kwao hali hiyo ni neema, kwani ndio mwanzo wa kukodisha mabuti kwa watu wanaotaka kuingia sokoni.

"Mtu anatoa shilingi 1000, anaacha viatu vyake na akimaliza mizunguko yake anarudisha buti na kupewa viatu vyake," anasema.

Johari Shaban, anasema kwa kipindi cha mvua, buti jozi moja inauzwa shilingi 12,000, lakini kwa kipindi cha jua kali, jozi ya buti inauzwa shilingi 8000.

Anasema katika biashara hapakosi changamoto, wapo baadhi ya wateja wanaoacha viatu vyao na kuondoka na buti zao.

Pia, anafafanua kuwapo baadhi ya vijana wanauouza mifuko na wanaongozana na wateja waliochukuwa buti na wakizunguka nao hurudi, hata wanarudisha mabuti na kuchukuwa viatu vyao.

Zuwena anasema katika kufanya biashara hiyo ya kukodisha viatu, wanazingatia masuala ya afya na kanuni zake, akitumia mifano mteja anapovaa buti, hupewa mfuko wa plastiki ambao aivae kwanza na kisha ndio anavaa buti.

Mhusika mwingine, Aisha Jamali, anasema katika kipindi cha mvua, huwa anajiongezea kipato pale watu wanapokuwa na matope miguuni, huwa anawaosha miguu na anapatiwa shilingi 200.

"Kimvua kikinyesha kidogo, soko linakuwa na matope, wateja wengine hawana uwezo wa kukodi buti, hivyo wanayakanyaga matope na kuja kwangu kuoshwa miguu kwa shilingi 200," anasema, akiongeza kuwa mvua ikinyesha kwao ni neema kutokana na kujiingizia kipato.

Hadi sasa, Soko la Mabibo ambalo liko ndani ya Manispaa ya Kinondoni, Dar es Salaam, limekuwa na mijadala mingi kutoka kwa umma, mojawapo ikiwa ni kuhusiana na hali ya mazingira yake yalivyo kirafiki.

Hata hivyo inavyojulikana, kasoro moja inafaa upande wa pili wa shilingi, kwani magumu yanayopatikana ndio inafungua nafasi ya ahueni ya kiuchumi kwa jamii mahali hapo wanatafuta kipato.

Inaelezwa kwamba, kumekuwapo ugumu katika uendelezaji soko hilo kutoka upande wa manispaa, kwa mamlaka husika haina milki rasmi ya eneo hilo, hivyo inashindwa kuendeleza na ndio moja ya sababu soko hilo linabaki katika hali hiyo inayosimuliwa miaka yote.

Mbali na hilo, Soko la Mabibo, Dar es Salaam limebaki kuwa na hadhi yake ya kuwa kituo kikuu cha kushusha ndizi ndani ya Dar es Salaam, kutoka mikoa tofauti inakozalishwa.

Kwa ujumla, bado kuna tafsiri masoko mengi ambayo ni kama wakala ndani ya Dar es Salaam, katika kushusha bidhaa na hasa vyakula, kama vile Temeke Stereo, Ilala, Soko Kuu la Kariakoo na Tandale.

# Apunguziwa kifungo miaka 30 hadi saba kumpa mimba mwanafunzi

**Na Kulwa Mzee**

MAHAKAMA Kuu Geita imemwondolea adhabu ya kifungo cha miaka 30 gerezani Masanja Elias, maarufu Mpini, na kuamuru atumikie kifungo cha miaka saba gerezani kwa kosa la kumpa mimba mwanafunzi wa kidato cha kwanza.

Hukumu hiyo ilitolewa juzi mbele ya Jaji Kelvin Mhina baada ya kupitia rufani ya kupinga adhabu ya kifungo cha miaka 30 gerezani iliyowasilishwa na Masanja na majibu ya mjibu rufani, Jamhuri iliyowakilishwa na Wakili Verena Mathias.

Mrufani alishtakiwa katika Mahakama ya Wilaya ya Mbongwe kwa mashtaka matatu, ikiwamo kumweka kinyumba mwanafunzi wa kidato cha kwanza mwenye umri wa miaka 16 na kumpa mimba.

Upande wa Jamhuri katika shauri hilo ulikuwa na mashahidi watatu na vielelezo vinne, upande wa mrufani, alijitetea mwenyewe kwa kiapo.

Binti katika ushahidi wake anadai mrufani ni mume wake, walianza uhusiano Juni 2023 na alipomwingilia mara ya kwanza aliahidi kumuoa.

Anadai mrufani alimpeleka kwa mama yake maeneo ya Masumbwe, wakaanza kuishi pamoja kama mke na mume kwa miezi miwili na kupata mimba.

Inadaiwa mama wa mrufani alimchukua binti na kumpeleka kupima ndipo alipokamatwa na kueleza kwamba ni mjamzito na mimba ni ya mrufani.

Ushahidi wa daktari ulidai kwamba Agosti 31, 2023 binti alipimwa na kubainika ana mimba ya miezi mitatu.

Mama mzazi katika ushahidi alidai binti yake ni mwanafunzi wa kidato cha kwanza, alizaliwa Mei mwaka 2005.

Shahidi wa tano ambaye ni mwalimu, alidai binti alijiunga na shule Januari 2023, alihudhuria masomo hadi Juni 2023 na Julai 2023 ilibainika ana ujauzito wa miezi miwili.

Baada ya kusikiliza shauri hilo hadi mwisho, mahakama iliona upande wa Jamhuri umethibitisha kosa na ilimtia hatiani mrufani na kumpa adhabu ya kutumikia kifungo cha miaka 30 gerezani.

Mrufani aliwasilisha hoja za rufani akiwa na sababu tatu ikiwamo mahakama ilikosea kumtia hatiani na kumpa adhabu ya kifungo cha miaka 30 gerezani bila kufanya vipimo vya DNA na hakuna shahidi aliyethibitisha kwamba mrufani ndiye alimpa mimba binti huyo.

Wakili wa mjibu rufani, Mathias alidai adhabu ya kifungo cha miaka 30 gerezani ilitolewa kwa mujibu wa sheria, ushahidi umethibitisha kosa dhidi ya mrufani na aliomba rufani yake itupwe haina mashiko.

Baada ya kusikiliza hoja za pande zote mbili, mahakama iliona kwamba mahakama ya chini haikutoa sababu za hukumu ambayo si ya lazima.

Jaji Mhina alisema mahakama ilitakiwa kuzingatia kuwa mrufani alikuwa mkosaji wa kwanza kwa kuwa hakuwa na rekodi ya uhalifu, alikuwa mlezi wa watoto watatu, tayari alitumia mwaka mmoja gerezani na alikuwa na umri wa miaka 25 na bado ana tija katika jamii.

"Katika hali hiyo, ninafuta na kuweka kando hukumu ya kifungo cha miaka 30 gerezani, mrufani alistahili msamaha kwenye adhabu badala ya kumpa adhabu ya juu.

"Mahakama inabadilisha adhabu ya miaka 30 jela na kumpa adhabu ya kutumikia kifungo cha miaka saba jela.

# MNH: Kisukari tishio kwa watoto wanaozaliwa

**Na Romana Mallya**

MKURUGENZI wa Huduma za Tiba Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), Dk. John Rwegasha, amesema watoto watatu kati ya 100 sawa na asilimia tatu wanazaliwa na tatizo la kisukari aina ya kwanza, huku Muhimbili pekee ikihudumia karibu 6,000.

Dk. Rwegasha aliyasema hayo juzi wakati akifungua mafunzo ya wiki mbili ya awamu ya pili kwa wauguzi kutoka nchi mbalimbali za Afrika wakiwamo Watanzania, yanayolenga kuwaongeza uelewa wa kuwahudumia watoto wenye kisukari aina ya kwanza.

Yanatolewa na Allied Healthcare Diabetes Educator Course for African Nurses (ADECA), kupitia udhamini wa kutoka Life for a Child kwa kushirikiana na International Society for Pediatric and Adolescent Diabetes (ISPAD).

Dk. Rwegasha alisema programu hiyo inadhaminiwa na watu kutoka Australia na Uingereza walioanzisha mpango wa kuwajengea uelewa wauguzi wanaowahudumia watoto wenye magonjwa hayo.

"Ukubwa wa tatizo kwa Tanzania ni karibu asilimia tatu, watoto watatu kati ya 100 wanazaliwa na tatizo la kisukari aina ya kwanza.

"Kwenye Chama cha Kisukari Tanzania (TDA) wanaohudumiwa Hospitali ya Muhimbili wamefikia karibu 6,000 kwa sababu elimu ya kutosha bado haijakuwapo.

"Asilimia tatu ni kubwa kama mtu anapoteza maisha bila kupata huduma wakati zinapatikana kwa urahisi," alisema.

Dk. Rwegasha alisema wanasisitiza na kuhamasisha mafunzo hayo kwa sababu ya uzito wa aina hiyo ya kisukari kwa watoto ambacho hurithi.

"Huwezi kufanya udhibiti kwa dawa peke yake au kudhibiti chakula kama ilivyo kwa kisukari aina ya pili," alisema.

Aidha, mtoto asipotibiwa anaweza kufariki dunia ndani ya muda mfupi kutokana na athari za kisukari na huishi kwa kupatiwa insulini.

Alisema mahitaji yao ni makubwa ikilinganishwa na kisukari cha watu wazima, bila kuwa na wataalamu wa karibu kusaidia, athari zinawanyemelea haraka ikiwa ni pamoja na kupofuka macho, presha na figo kushindwa kufanya kazi.

"Madaktari wana uelewa wa kutibu tatizo hili, lakini sasa na wauguzi ambao hukaa na wagonjwa muda mrefu lazima wajengewe uwezo," alisema.

Alisema wakishafuzu mafunzo hayo watakuwa sehemu ya kuwajengea uwezo wenzao na kikubwa ni kuongeza ubora wa huduma.

Kuhusu madaktari, Dk. Rwegasha alisema mwongozo wa Shirika la Afya Duniani (WHO) unataka wagonjwa 4,000 kwa daktari mmoja, lakini kwa Tanzania hali ilivyo ni wagonjwa 20,000 kwa daktari mmoja.

"Muhimbili tupo katika mpango wa kuendeleza kitengo cha hospitali ya watoto, kwa sasa tupo katika kujengeana uwezo kwa madaktari watoto na kutoa mafunzo kwa wauguzi ili kwenda sambamba na madaktari," alisema.

Kuhusu changamoto za kuhudumia watoto, Dk. Rwegasha, alisema ni uelewa wa wazazi au walezi wa namna ya kukaa na watoto na wakati gani na kuwapa insulini na aina ya vyakula, hivyo huchangia uwezekano ugonjwa kulipuka kwa mtoto. Mkurugenzi wa Mafunzo hayo kutoka ADECA, Dk. Chizo Agwu, alisema mafunzo hayo ni muhimu kwa wauguzi kwa sababu yanasaidia pia, familia zenye watoto kujengewa uelewa wa kuwahudumia.

Alisema awamu ya kwanza ilitoa mafunzo kwa wauguzi 15 kutoka nchi saba na awamu ya pili inahusisha pia, wauguzi 15 kutoka nchi tisa za Kusini mwa Jangwa la Sahara, Watanzania wakiwa wawili.

Dk. Anicetu Muchunguzi, anayeishi na kisukari aina ya kwanza takribani miaka 11 na Makamu Mwenyekiti wa Umoja wa Vijana Wanaoishi na Kisukari aina ya kwanza Tanzania (TDYA) alisema:

"Vijana wengi wenye zaidi ya miaka 25 wanapoteza maisha kwa sababu hawana uwezo wa kugharamia matibabu yao na pia, hawajajengewa uwezo wa kujitegemea tangu wadogo.

Aliiomba serikali ilichukulie suala hilo kwa uzito kwa sababu kila kijana mwenye kisukari ana haki ya kuwa na afya njema na kuishi huku wadau wakisaidia kuleta nuru.

Dk. Rachel Nungu, kutoka TDA, alisema wauguzi wanapewa mafunzo hayo ili kujua kuishi, kuongea na kuwashauri watoto wenye kisukari aina ya kwanza kwa sababu hukaa na watoto muda mrefu katika vituo vya afya.


Ofisa Muuguzi kutoka Hospitali ya Rufani Bugango, Mwanza, Philipines Katama, ambaye ni miongoni mwa wanufaika wa mafunzo hayo, alisema watoto wana changamoto nyingi katika kudhibiti kisukari na kuweza kuzuia matokeo tata.

"Mojawapo ya changamoto tunazopata ni katika ufundishwaji watoto, wazazi au walezi ili kudhibiti kisukari. Maeneo mojawapo ambayo ni changamoto ni katika ulaji unaoweza kufaa kudhibiti, matumizi ya dawa na mazoezi. "Jambo jipya nililopata kupitia mafunzo haya ni namna ya kurekebisha dozi kulingana na chakula anachopata mtoto na kulingana na mazingira yake," alisema.



Mratibu Mteule wa Taasisi ya Kiislamu ya TAAWANU Mkoa wa Dar es Salaam, Abdulqadir Kajumulo (wa pili kushoto), akitoa neno la shukrani kwa Uongozi wa Taasisi hiyo Kimataifa na Kitaifa, baada ya kutangazwa kushika nafasi hiyo, wakati wa hafla ya chakula cha usiku, mkoani humo juzi, iliyoandaliwa na TAAWANU, kwa kinamama kutoka mikoa saba ya Tanzania Bara na Zanzibar ambao wapo kwa mafunzo ya wiki moja ya ujasiriamali, kujitambua na kuwawezesha vitendea kazi ili wajikwamue kiuchumi. Kutoka kulia ni Mwenyekiti wa Taasisi hiyo Kimataifa, Zahara Dattan, Mwenyekiti Taifa, Alhaji Sheikh Hashimu Kamgunda, Mtoa Mada kutoka nchini Uingereza, Sheihk Abdul Muiid na viongozi wengine.
**PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## KABWELA Na Fadhili Mohammed



# Walia mkwamo marekebisho Sheria ya Ndoa

**Na Elizabeth Zaya**, SHINYANGA

BAADHI ya wadau kutoka mashirika yanayounda Mtandao wa Kutokomeza Mimba za Utotoni (TECMN), wameomba serikali kuandika muswada wa maboresha ya Sheria ya Ndoa na kuuwasilisha katika mkutano ujao wa Bunge ili ujadiliwe na kufanyiwa maboresho rasmi.

Wakizungmza na Nipashe kwa nyakati tofauti wakiwa kwenye ziara maalum ya kutoa elimu ya kupambana na kutokomeza ndoa hizo za utotoni mkoani Shinyanga, wadau hao walisema licha la mahakama kutoa amri ya kufanya mabadiliko sheria hiyo ya mwaka 1971, hakuna kilichofanyika hadi sasa.

"Tunafahamu kwamba baadhi ya vyanzo vya ndoa hizo za utotoni ni umaskini wa familia, hivyo zinashawishika kuozesha watoto wao mapema kwa sababu ya kutafuta kipato.

"Wanawafanya watoto wao kama chanzo cha mapato, wakisahau kwamba wanawaingiza katika matatizo," alisema Adamu Mkaka, Mkuu wa Idara ya Ulinzi na Usalama wa Mtoto wa Shirika la Plan international.

"Tatizo lingine kubwa linalochangia watoto wadogo waendelee kuozeshwa ni kuchelewa mabadiliko ya sheria hii. Kama tutarekebisha sheria, itasaidia kwa sababu zipo familia zina hali nzuri ya kiuchumi, lakini kwa sababu sheria inawapa mwanya wa kuwaozesha kwa umri huo basi na wao wanafanya," aliongeza.

Mkaka alisema mkwamo uliopo kwenye mabadiliko ya sheria hiyo unachangia hali izidi kuwa mbaya zaidi.

"Tunachoomba kwa sasa ni Waziri wa Sheria na Katiba ashirikiane na Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, waandike huo muswada wa mabadiliko ya sheria hiyo na wapeleke bungeni, wabunge waujadili ili upitishwe rasmi ili tulinde watoto na janga hili.

**"Wanawafanya watoto wao kama chanzo cha mapato, wakisahau kwamba wanawaingiza katika matatizo," alisema Adamu Mkaka, Mkuu wa Idara ya Ulinzi na Usalama wa Mtoto wa Shirika la Plan international.**

"Ninachoomba kwa wabunge na mawaziri wa kisekta hili jambo tulipeleke kwenye Bunge lijalo, tulimalize, kwa sababu tulishafikia pazuri, wanavyozidi kuchelewesha ndivyo watoto wengi wanavyozidi kupata madhara.

"Kwa sababu wanatakiwa wajue kwamba kinacholindwa hapa ni kizazi cha watoto wa Tanzania, hivyo kuendelea kuwa na kizazi cha watu wengi wanaopata mimba za utotoni tunatengeneza kizazi ambacho si productive (hakizalishi) lakini tunazalisha madhara mengi zaidi kwa taifa," alisema.

Neema Abeid, Ofisa Mbunifu na Kujenga Uwezo kutoka Shirika la Medaa ambao ni wanachama wa mtandao huo wa kutokomeza ndoa za utotoni, alisema wanashindwa kuelewa sababu za kushindwa kuheshimu amri ya mahakama iliyotaka sheria hiyo ibadilishwe.

"Mahakama ni muhimili muhimu na unaoaminika kwa kutoa haki, tunaomba uamuzi wake uheshimike na kuzingatiwa, sheria ya ndoa ibadilishwe.

"Ikumbukwe kwamba vifungu vinavyolalamikiwa vya sheria hiyo ya ndoa ambavyo mahakama hiyo iliamuru vibadilishwe, ni vya 13 na 17 vinavyoruhusu mtoto wa miaka 14 na 15 kuolewa kwa ridhaa ya wazazi na amri ya mahakama.

## Tulia: Ushirikiano IPU, UN ni muhimu kuimarisha mustakabali wa dunia

**NEW YORK,** MAREKANI

SPIKA wa Bunge la Tanzania na Rais wa Umoja wa Mabunge Duniani (IPU), Dk. Tulia Ackson, amethibitisha kuwa ushirikiano endelevu baina ya IPU na Umoja wa Mataifa (UN) ni muhimu katika kutekeleza ajenda mbalimbali za pamoja kwa manufaa ya dunia.

Dk. Tulia alitoa kauli hiyo jana alipowasilisha hotuba ya IPU katika Mkutano wa UN wa Wakuu wa Nchi na Serikali uliojadili mustakabali wa dunia kwa siku zijazo (Summit of the Future), uliofanyika katika Ofisi za UN jijini New York, Marekani.

Akiwasilisha hotuba yake, Dk. Tulia alieleza kuwa kwa zaidi ya robo karne tangu kuanzishwa Azimio la Milenia, ushirikiano kati ya IPU na UN umeonesha mafanikio makubwa, kila mwaka wakifikia malengo ya kuiwezesha UN kuwa taasisi inayowajibika, yenye uwazi na inayotekeleza maazimio yake ipasavyo.

Dk. Tulia alibainisha kuwa nafasi ya mabunge imeainishwa wazi katika lengo namba 55 la Azimio la Pact of the Future, ambalo linaelekeza kuimarisha ushirikiano kati ya mabunge na UN.

Akisisitiza umuhimu wa wajibu wa mabunge, Dk. Tulia alinukuu maneno ya Baba wa Taifa la Tanzania, Hayati Mwalimu Julius Nyerere, aliyesema "Inawezekana, tekeleza wajibu wako", akiongeza kuwa IPU inatimiza wajibu wake kuhakikisha kuwa UN inaendelea kuwa imara kupitia mabunge.

"Dunia inahitaji mabadiliko na sehemu pekee ya kufanya mabadiliko hayo ni ndani ya UN, na wakati wa kufanya hivyo ni sasa," alisisitiza Dk. Tulia.



Madaktari Bingwa wa Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI), wakifanya upasuaji wa moyo katika Hospitali ya Taifa ya Moyo ya Zambia jana, kwa kushirikiana na wataalamu wa hospitali hiyo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Madaktari bingwa wa moyo JKCI waenda Zambia kufanya upasuaji

**Na Joseph Mwendapole**

MADAKTARI bingwa wanne wa moyo wa Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI) wamewasili Zambia na wameanza kufanya upasuaji kwa wagonjwa wenye matatizo ya moyo katika nchi hiyo.

Timu hiyo ya madakari hao itashirikiana na wenzao wa Hospitali ya Taifa ya Moyo ya Zambia na watafanya upasuaji wa moyo kwa muda wa wiki moja.

Mkuu wa msafara huo, Dk. Viviane Mlawi wa JKCI ambaye ni daktari bingwa wa moyo kwa watoto, alisema timu yao imeambatana na mtaalamu mbobezi wa chumba cha upasuaji na mtaalamu wa usingizi katika upasuaji moyo.

Alisema wameambatana pia na mbobezi katika kuhudumia wagonjwa wa nje wanaokuja kupata matibabu Tanzania, Dk. Maiyer Msengi na wauguzi wawili ambao ni wabobezi wa chumba cha wagonjwa mahututi (ICU).

Dk. Mlawi alisema malengo makubwa ya safari hiyo ni matano ambayo ni kufanya upasuaji wa moyo kwa wahitaji ambao ni wengi Zambia na kuwajengea uwezo madaktari wa Zambia kuhusu mbinu za upasuaji ambazo hawajawa nazo na kubadilishana ujuzi.

Alitaja lengo lingine ni kukagua kwa pamoja na kubainisha maeneo ambayo Tanzania inaweza kushirikia na Zambia katika kuwasaidia wananchi wa Zambia kupata matibabu ya kibingwa kwa wepesi na gharama nafuu. Dk. Mlawi alisema madaktari hao watakagua na kubainisha vifaa tiba ambavyo vipo na vile ambavyo havipo ili kuweka mikakati ya jinsi gani wanaweza kushirikiana kuvipata ili kuboresha huduma zao. Alitaja lengo lingine kuwa ni kuona maeneo mbalimbali ya ushirikiano katika utafiti, teknolojia na mambo ya msingi ambayo Tanzania iko mbele katika eneo hilo kwa ukanda huu wa Afrika Mashariki na Kati.

Dk. Maiyer ambaye ni mtaalamu wa usimamizi wa wagonjwa kutoka nje ya nchi, alisema yapo mambo mengi ambayo JKCI na Hospitali ya Taifa ya Moyo Zambia wanaweza kuyafanya kwa kushirikiana kwa ajili ya maendeleo ya nchi hizo mbili.

Alitaja masuala hayo kuwa ni pamoja na kuhakikisha wanarahisisha utoaji vibali vya kuingia katika nchi hizo (visa), malazi kwa wanaotembelea nchi hizo na usajili wa mawasiliano ya namba za simu na vibali vya kwenda kupata matibabu. Alisema kwa upande wa Tanzania watahakikisha kunakuwa na uhakika wa miadi ya kukutana na madaktari bingwa na kupata huduma kwa wakati ili kupunguza gharama za kuishi nchini kwa muda mrefu.

Alisema watahakikisha pia kunakuwa na huduma bora wakati na baada ya upasuaji wa wagonjwa wa moyo na kufanya JKCI iendelee kuwa kimbilio la mataifa mengi ya Afrika na kwingineko.

Alisema jambo lingine la msingi ambalo watahakikisha linazingatiwa ipasavyo ni uhakika wa gharama sahihi za vipimo na matibabu na usalama wa mgonjwa kwa kulinda haki zake zote akiwa anapata matibabu.

Alisema kuna umuhimu wa kuendelea kuboresha uhusiano baina ya mataifa hayo mawili katika utoaji taarifa ubalozini, hasa kwa kuzingatia kuwa kuna mahitaji makubwa ya watu kuja nchini kupata matibabu ya moyo.

Msemaji wa Hospitali ya Moyo ya Taifa ya Zambia, Dk. Chabwela Shumba, alisema wamekutana na madaktari wa Tanzania na baada ya kufanya uchambuzi wa uwekezaji ambao serikali imefanya kwa JKCI, wameona watanufaika kwa kiwango kikubwa kama watashirikiana na Tanzania.

"Tumeshangaa sana kuona uwekezaji mkubwa uliofanywa katika vifaa vya kisasa kama MRI, CT SCAN, rasilimali watu, teknolojia na kiwango kikubwa cha wagonjwa waliofanyiwa upasuaji wa moyo kwa mafanikio makubwa," alisema Shumba.



## HABARI KASKAZINI

# TCB yatamani vijana wauze kahawa Dubai

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

BODI ya Kahawa Tanzania (TCB), imesema inatamani kuona vijana wa kitanzania wanapata fursa ya kufungua migahawa ya kisasa ya unywaji wa kahawa katika Jiji la Dubai lililoko Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE) kama nchi jirani zilivyofanikiwa kwenye hatua hiyo.

Akizungumza jana na Nipashe katika mahojiano maalum kuhusiana na ushindani wa nchi za Afrika ya Mashariki zinazozalisha kahawa, Mkurugenzi Mkuu wa Bodi ya Kahawa Tanzania (TCB), Primus Kimaryo, alisema kuna mwitikio mkubwa hivi sasa; baada ya kuona wenzao wa nchi za jirani, vijana wao wanakwenda mpaka Dubai, wanakwenda nchi mbalimbali kufanya kazi hiyo.

Mshindani mkuu wa Tanzania, kama nchi za Afrika ya Mashariki zinazolima kahawa kwa wingi ni Uganda, Kenya, Rwanda na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC).

**"Tunahitaji kutoa ajira kwa vijana wetu. Katika mnyororo wa thamani kwenye 'hospitality industry' ni eneo kubwa sana, ambalo vijana watajifunza kutoa huduma, kutayarisha...**

"Tunahitaji kutoa ajira kwa vijana wetu. Katika mnyororo wa thamani kwenye 'hospitality industry' ni eneo kubwa sana, ambalo vijana watajifunza kutoa huduma, kutayarisha kikombe kilicho bora, kujifunza kuonja kahawa, kujifunza ni namna gani ya kutayarisha vikombe vya kahawa na hasa maeneo ya hotelini.

...Hii ni ajira kubwa ambayo tukiifanya vizuri vijana wetu watapata fursa ya kuajiriwa katika sekta ya kahawa kwa upana wake."

Alisema licha ya Tanzania kulima kahawa zaidi ya asilimia 93 inayokwenda nje, unywaji wa kahawa bado unasuasua kwa asilimia saba.

Aidha, alisema tija katika sekta ya uzalishaji wa kahawa nchini, inatishiwa na mambo tisa yanayosubiri mkono wa serikali na juhudi za wadau walioko kwenye mnyororo wa thamani kupata ufumbuzi wa kudumu wa namna bora ya kuinua uzalishaji wa zao hilo la kimkakati.

Kwa mujibu wa kanzidata ya TCB, kaya 400,000 Tanzania zinalima kahawa, huku asilimia 90 ya wazalishaji wa zao hilo wakiwa ni wakulima wadogo.

Pia Tanzania inategemea uzalishaji wa zao hilo katika hekta 220 zilizoko katika mikoa 17.



Mkuu wa Mkoa wa Manyara, Queen Sendiga (katikati), akizungumza na mchimbaji maarufu wa madini ya Tanzanite, Bilionea Saniniu Laizer (kushoto) na Mkuu wa Wilaya ya Simanjiro, Fakii Lulandala, alipotembelea Shule ya Msingi Saniniu Laizer, katika Kijiji cha Naepo, Kata ya Naisinyai, iliyojengwa na Bilionea Laizer na kuikabidhi serikali, juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# Hifadhi za miti ya mikoko kuwa utalii wa ikolojia

**Na Oscar Assenga,** TANGA

WIZARA ya Maliasili na Utalii, inafikiria kuzitumia hifadhi za miti asili ya mikoko kama utalii wa kiikolojia ambao una tija kiuchumi kwa jamii inayozunguka hifadhi hizo katika mwambao wa Mkoa wa Tanga.

Kutokana na umuhimu wake kiuchumi, Naibu Katibu Mkuu wa Wizara hiyo anayeshughulikia utalii, Nkoba Mabula, alisema serikali itaendelea kuhamasisha upandaji wa mikoko katika mkoa huo, kwa ajili ya biashara ya kaboni na kusaidia kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi.

"Mwambao wa Tanga na maeneo mengine ya Pwani, yanapata changamoto ya kuliwa na maji ya bahari kutokana na kina kuongezeka; lakini yana faida kwa jamii yetu, hasa biashara ya kaboni.

Zaidi aliongeza: "Katika baadhi ya maeneo mikoko inachukuliwa na maji, hivyo inasababisha kingo za bahari kumong'onyoka hivyo maji huingia nchi kavu na kusababisha mafuriko.

...Bahati nzuri mikoko hii sasa ni utalii ikolojia ambao, hauleti tu faida kwa jamii, bali pia unasaidia katika kuwafanya watu wa maeneo haya kutambua umuhimu wa kuhifadhi rasilimali zao za asili."

Akiwa mkoani Tanga, Mabula, alitembelea na kukagua hifadhi za mikoko, magofu ya Tongoni na Shamba la Miti Longuza linalomilikiwa na Wakala wa Misutu Tanzania (TFS).

Mabula, alisema maeneo ya mashamba na misitu ya serikali, yanaweza kuimarishwa kwa kuboresha miundombinu ya utalii, kwa kutengeneza mikakati ya masoko ili kukuza shughuli za utalii.

Alisisitiza uwekezaji mkubwa unaoendelea kufanywa na TFS, hasa kwenye mikoko iliyopo pembezoni mwa Tanga Beach, Tongoni na Shamba la Miti Longuza mkoani Tanga, unahitaji kuambatana na hadithi zenye kuvutia zinazoweza kutangaza utalii wa misitu na malikale, huku zikiweka bayana umuhimu wa kulinda mifumo ya ikolojia.

Kamanda wa Uhifadhi Kanda ya Kaskazini, James Nshare, aliahidi pia kuimarisha ushirikiano kati ya ofisi zote za TFS na wadau mbalimbali katika kukabiliana na changamoto za uhifadhi, hususani moto, ambao ni moja ya changamoto kuu katika mashamba na misitu ya hifadhi.

Alisema: "Wenzetu kwenye halmashauri wana sheria ndogo za kuzuia moto kuanzishwa ndani ya misitu, pia sheria yetu ya misitu inawataka watu kushiriki kuzima moto unapotokea. Ni muhimu tushirikiane katika kukabiliana na majanga ya moto."

# Mchakato uanzishaji Bodi ya Mawasiliano na Uhusiano waiva

**Na Woinde Shizza,** ARUSHA

SERIKALI imesema mchakato wa uanzishaji wa Bodi ya Kitaifa ya Mawasiliano na Uhusiano ya Umma, umeiva.

Naibu Waziri wa Habari na Mawasiliano, Maryprisca Mahundi, alisema hayo jana jijini Arusha, wakati akifungua mkutano wa Jumuiya ya Maofisa Mahusiano ya Umma ya Afrika Mashariki (EAPRA).

Mkutano huo unawajumuisha wataalamu na viongozi kutoka sekta ya mawasiliano na uhusiano ya umma kutoka nchi saba za Afrika ya Mashariki.

"Serikali iko mbioni kushirikiana na wadau wa sekta hii, kuunda sheria itakayowezesha kuanzishwa kwa Bodi ya Kitaifa ya Mawasiliano na Mahusiano ya Umma, ambayo pamoja na mambo mengine itasaidia taaluma hii kupata msukumo wa kisheria.

...Na kuwa na mifumo ya usimamizi kama ilivyo kwa taaluma nyingine muhimu kama vile sheria na uhasibu. Hii ni kwa sababu taaluma ya mawasiliano na uhusiano wa umma, inazidi kupata umuhimu mkubwa katika ulimwengu wa sasa, ambapo uwazi, uaminifu, na mawasiliano yenye manufaa yamekuwa sehemu muhimu ya maendeleo ya kijamii na kiuchumi."

Alisema kuwa EAPRA, inabaki kuwa kiini muhimu cha kuhakikisha kuwa wataalamu wa mawasiliano wanapata nafasi ya kujenga sauti imara katika vikao vya maamuzi Afrika Mashariki.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa EAPRA na Rais wa Chama cha Maofisa Uhusiano ya Umma Tanzania, Assah Mwambene, alisema mkutano huo utafungua njia mpya kwa taaluma hiyo kuingizwa kwenye meza za maamuzi na kushiriki katika mchakato wa sera, ndani ya ukanda wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Alisema kuwa uamuzi wa kufanya Arusha kuwa makao makuu ya EAPRA, uliofanywa mwaka 2022 katika mkutano uliofanyika Mombasa, Kenya, ndiyo uliofanikisha kuimarika kwa taaluma hiyo.

Mmoja wa washiriki ambaye ni Mwenyekiti wa Jukwaa la Wahariri Tanzania (TEF), Deodatus Balile, alisema maofisa uhusiano wana kazi kubwa ya kuhakikisha kwamba wanatangaza taasisi zao na siyo kubeba mikoba ya mabosi zao.



# ‘Bifu’ kati ya mgodi, wananchi lamalizwa

**Na Samson Chacha,** TARIME

MGOGORO uliokuwapo kwa muda mrefu baina ya mgodi wa Barick North Mara uliopo Nyamongo, Tarafa ya Ingwe wilayani Tarime mkoani Mara pamoja na wananchi wanaoishi maeneo jirani na mgodi huo umemalizika.

Mgogoro huo ulisababisha kundi la vijana katika maeneo hayo kuvamia mara kwa mara mgodini hapo na kuiba mawe yanayosadikiwa kuwa ya dhahabu na wengine kudaiwa kuuawa wakiwa ndani ya mgodi kwa kupigwa risasi na walinzi.

Mgogoro huo ulimalizika juzi, uongozi wa mgodi huo kuwakusanya vijana kutoka vijiji 11 vilivyo jirani na mgodi kushiriki michezo pamoja.

Katika michezo hiyo, Mkuu wa Wilaya ya Tarime, Meja Edward Golewe, aliagiza kuwepo kwa ushirikiano wa kudumu baina yao ili migogoro hiyo isijirudie.

Meja Golewe alisema miongoni mwa vitu vilivyobabisha kufifia kwa uhusiano huo ni pamoja na uvamizi wa mgodi pamoja na uporaji wa mawe hali iliyosababisha mauaji ya vijana na nguvukazi ya maeneo hayo.

“Hii ni hatua nzuri mliofikia Barick kwani kombe hili la Mahusiano Cup litasaidia sana katika kurejesha maendeleo katika eneo hili kwani migogoro inarudisha nyuma maendeleo,” alisema Meja Golewe.

Katika hatua nyingine, Meha Golewe aliiagiza halmashauri hiyo kuelekeza zaidi ya Sh.bilioni tisa zinazotolewa kama sehemu ya huduma kwa jamii katika miradi iliyopangwa na iliyokusudiwa kutekelezwa siyo vinginevyo ikiwamo miradi ya maji, elimu, afya na barabara.

Meneja wa mgodi huo, Apolinary Lyambiko, alisema walifikia hatua hiyo kutokana na hapo awali kuwapo kwa makundi ya vijana waliojihami kwa silaha za jadi kuvamia mgodi na kupora mawe ya dhahabu pamoja na kuwajeruhi walinzi, kuharibu miundombinu ya mgodi.

Alisema vijana hao walikuwa wakiharibu mabomba ya maji na kukwamisha shughuli za maendeleo.

Ofisa Mtendaji wa mgodi huo, Dk. Mark Bristow, aliahidi kujenga uwanja wa kisasa wa michezo katika Kata ya Matongo ambao utatumika katika michezo na kuwa chanzo cha mapato katika kata hiyo.

Kadhalika alihimiza kuendelezwa kwa uhusiano ulipo sasa ili waendelee kunufaisha jamii pamoja na taifa.

# Kituo cha afya chajengwa miaka 12, hakijakamilika

**Na Marco Maduhu,** KISHAPU

UJENZI wa Kituo cha Afya Bubiki, umeelezwa kushindwa kukamilika kwa zaidi ya miaka 12 sasa na kusababisha wananchi kukosa huduma za matibabu.

Hayo yalibainishwa juzi na Ofisa Kilimo wa Bubiki, Juma Magesa, wakati akisoma taarifa kwa niaba ya Mtendaji wa Kijiji hicho katika mkutano wa hadhara wa Mbunge wa Kishapu, Boniphace Butondo.

Alisema wananchi wanakabiliwa na kero ya upatikanaji wa huduma za afya licha ya kujitolea kuanza ujenzi wa kituo hicho ambako ni zaidi ya miaka 12 sasa bado hakijakamilika huku wananchi wakilazimika kufuata huduma hiyo katika vijiji vya jirani.

Magesa alisema ujenzi wa kituo hicho ulianza mwaka 2012 na sasa umefikia hatua ya renta, lakini awali Mbunge Butondo alitoa msaada wa mifuko 100 ya saruji ili kuendeleza ujenzi huo, lakini ilibadilishiwa matumizi na kuelekezwa kwenye ujenzi wa nyumba za walimu.

Mbunge wa Kishapu, Boniphace Butondo, alisema kutoka na kufahamu umuhimu wa huduma za afya kwa jamii, hivyo ameamua kuchangia tena mifuko 100 ya saruji ili kusukuma ujenzi wa kituo hicho, huku akitoa angalizo kwamba mifuko hiyo isibadilishwe matumizi.

**“Ujenzi wa kituo hiki cha afya sasa nalivalia njuga, haiwezekani uchukue muda kukamilika tangu mwaka 2012, na kata hii ina watu wengi lakini hakuna huduma za afya,” alisema**

“Ujenzi wa kituo hiki cha afya sasa nalivalia njuga, haiwezekani uchukue muda kukamilika tangu mwaka 2012, na kata hii ina watu wengi lakini hakuna huduma za afya,” alisema Butondo.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Kishapu, Emmanuel Johnson, alipopigiwa simu na Mbunge juu ya hatua ambazo serikali imezichukua kukamilisha ujenzi wa kituo hicho, alisema kwamba tayari walishaiombea bajeti yake serikali kuu.

Kadhalika alisisitiza kwamba endapo wakikwama kupata fedha hizo, mwaka ujao wa fedha wataitengea bajeti kupitia mapato ya ndani.

Diwani wa Kata wa Bubiki, James Kasomi, alisema kata hiyo ina jumla ya wananchi 15,000 na kwamba wanatumia Zahanati ya Nyasamba kupata huduma ambayo ina watumishi watatu.

Hivyo alimuomba Mbunge pamoja na serikali kusaidia kukamilisha ujenzi wa kituo hicho ili kuboresha huduma za matibabu kwa wananchi.

Baadhi ya wananchi wa Kata ya Bubiki walisema kukosekana na huduma za afya wamekuwa wakipata shida ya kupata matibabu hali inayowalazimu kwenda kwenye kata za jirani ikiwamo Busangwa.



Abiria wakishuka katika kivuko cha MV Mara, eneo la Kurugee, kinachounganisha Musoma Vijijini na Mwibara, mkoani Mara, juzi. Kwa mijibu wa abiria, gati la kivuko hicho, linaonekana kujengwa chini ya kiwango na kusababisha lifunikwe na maji. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wazee wa kimila wakubaliana kutokomeza ukatili

**Na Timothy Itembe,** TARIME

WAZEE wa kimila kutoka koo 13 za jamii ya Wakurya wilayani Tarime mkoani Mara wamekubaliana kutokomeza mila potofu zinazoendekeza masuala ya ukatili.

Vilevile wameiomba serikali kudumisha amani na kudhibiti wizi katika maeneo yao.

Walisema hayo juzi katika mkutano wa pamoja na Mkuu wa Wilaya ya Tarime, Edward Ngowele, uliolenga kudhibiti ukatili wa kijinsia ukiwamo ukeketaji, ubakaji pamoja na vipigo kwa wanawake.

Katibu wa koo hizo, Sinda Nyasibora, alisema wazee wamekubaliana kutokomeza vitendo hivyo ikiwa ni pamoja na kutoa ushirikiano katika serikali ili kudhibiti kabisa matukio ya namna hiyo.

Aidha, alisema kwa sasa katika maeneo yao kuna ongezeko la wizi wa mifugo ambao unarudisha nyuma maendeleo katika koo hizo, hivyo kuomba msaada wa haraka kutoka katika vyombo vya ulinzi na usalama.

Naye Nashoni Marwa alisema upo umuhimu wa kuweka mkakati wa pamoja kwa wazee wa mila kutoka koo hizo kuhakikisha wanakabiliana na ukatili huo unaotajwa kuendelea katika maeneo yao.

Kadhalika, alisema sambamba na kudhibiti vitendo hivyo wanatakiwa kujadili mikakati ya kudumisha amani kwa wananchi wa Tarime na taifa kwa ujumla.

Ngowele aliwataka wazee hao kuwa kiungo muhimu katika kuleta amani wilayani humo sambamba na kuhakikisha vitendo vya ukatili vinatokomezwa, kwamba wao ndiyo nguzo kwa jamii hizo.

ama
ALHAMISI SEPTEMBA 26, 2024
AFYA NA MAZINGIRA



Ukurasa 12

**Fahamu operesheni ya kuwakimbiza tembo shambani wakilishwa pilipili**






Ukurasa 13

**Majaliwa asafiri na ajenda Mazingira ya Rais; Kijaji anuia Azimio Dodoma**

AFYA

# Simulizi ya Mwenyekiti wa Wagumba alivyotaka kuiba mtoto, akashindwa

- Safari ya kuolewa, kuachika ndoa mbili...
- Kipigo hadi kuzimia, kisa kashfa mtoto
- Uzoefu wa kukosa 'haki', licha kuhitaji
- Bei ndogo upandikizaji mimba Mil. 13/-

**Na Christina Mwakangale**

SHAMILA Makwenjula, kwake hali ya ugumba inamfanya atafsiri dhana tofauti kwenye jamii, anapokabili hali anayoishi nayo kutokuwa na mtoto.

Hatua za unyanyapaa, kutodumu katika ndoa mbili alizopitia, kumemsababishia hisia kali na hata kuthubutu jaribio la kuiba mtoto.

Mzaliwa huyo wa mwaka 1973 katika kijiji cha Mtimbila, mkoani Morogoro, ameisimulia Nipashe wastani wa wiki mbili sasa, baada ya huduma ya upandikizaji mimba (IVF) kuzinduliwa katika Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH).

Shamila kwa sasa ni Mwenyekiti wa Chama cha Wagumba Tanzania (CCWTZ), wazo lililoanza mwaka 2015, ila usajili na shughuli rasmi zilianza mwaka 2022, jumla ya wanachama sasa ni 600.

Anaueleza umoja wao ni mkusanyiko wa kinamama na kinababa wenye tatizo la ugumba na tasa, ajenda yao na kubadilishana mawazo na kupeana moyo, katika kulikabili tatizo lao kijamii na kitaifa.

Shamila anaeleza wanachama wengi ni wagumba ambao wanatibika, ila walio tasa hawatibiki kisayansi.

### SHAMILA NI NANI


Huyo pia ni mjasiriamali, anayesimulia maisha yake alioléwa akiwa na umri wa miaka 23 na baada ya miaka mitatu akaachika. Mwaka 1995, akaolewa tena na kudumu katika ndoa miaka 11 hadi mwaka 2006, akaachika tena.

"Kuna mwaka nikiwa Dar es Salaam akili ilinituma niibe mtoto. Niliondoka kijijini, nikasema kwa kipindi cha miezi tisa hadi nitakaporudi watajuwa nilikuwa mjamzito, kumbe kwa muda huo nilipanga kuiba mtoto," anasema.

Hata hivyo, anasema alikwamishwa na mambo makuu mawili; alishindwa kupata mtoto wa kuiba katika kipindi anajifanya na ujauzito miezi tisa, pia baadaye ikamjia hisia za kibinadamu namna angemtesa mwenye mtoto kisaikolojia.




Kituo cha Upandikizaji Mimba, kilichofunguliwa hivi karibuni katika Hospitali ya Taifa Muhimbili, Dar es Salaam. **PICHA ZOTE: CHRISTINA MWAKANGALE**



Shamila Makwenjula

Shamila anaisimulia Nipashe, kwa muda mrefu hamu yake kuitwa 'mama' haijamtoka hasa alipokuwa kwenye ndoa na amefanya malezi ya watoto wa nduguze kama mbadala apate mtazamo chanya kwenye jamii, lakini bado azma yake kuwa mlezi halisi wa kudumu haikutimia.

"Ukiwa na mtoto, kwanza katika familia au jamii ni kama heshima fulani. Wagumba tunapata hisia kali sana na hata msongo wa mawazo, watoto ni faraja.

"Wakati mwingine ukiwa nao ni ulinzi kwa familia ulikoolewa. Ebu fikiria umeolewa nyumbani hakuna watoto, mawifi, mama mkwe sijui wanakuonaje?

"Hata urithi utaachiwaje na mume, familia ulikoolewa wanakuona huna mchango wowote, ndio maana kuna kesi nyingi za mali kuhusu wanandoa," anasema Shamila. Hata hivyo, kisheria, kuna haki za msingi za mke.

Mama huyo analalamika: "Tunaonekana hatujakamilika, wenye laana, mikosi, manyanyaso kama nilivyosema, ukiwa mke mwenza ndio usiseme! Ndio maana nikapata wazo la kuiba mtoto, hii sio siri ila nikawaza nitakayemwibia atajisikiaje?

### ANGEMNYONYESHA VIPI?

Anaendeleza simulizi: "Kuhusu kumnyonyesha mtoto ambaye ningemuiba, maziwa ningeyapata kwa gharama yoyote. Kijijini

INAENDELEA UK.14

MAZINGIRA

# Fahamu operesheni ya kuwakimbiza tembo shambani wakilishwa pilipili

• Makali yake 'wamekoma' mwaka mzima wanabaki hifadhini




Shughuli za upandikizaji pilipili kudhibiti tembo kutoka hifadhini Mikumi, kuingia katika mashamba ya watu. **PICHA ZOTE: MPIGAPICHA WETU**

**Na Francis Ndemela**

UVAMIZI wa tembo katika mashamba ya wakulima wengi nchini imekuwa kilio kikubwa kwa wakulima na watu wanaoishi maeneo ya pembezoni mwa hifadhi, mbuga na hata mapori tengefu.

Hiyo ni kutokana na wanyama katika maeneo hayo wanaingia katika makazi ya watu, kisha wanavamia mashamba na kufanya uharibifu, hususani kwa mazao ya chakula, kujeruhi na hata kuua watu.

Imekuwa changamoto kubwa kwa wakazi na wakulima wanaoishi maeneo hayo, wakibuni mbinu za kukabiliana na wanyama hao kulinda uhai wao, mashamba na kuzuia uharibifu unaofanywa na tembo.

Kuna jitihada zimekuwa zikifanywa na wataalamu wa mazingira, pia kwa wanyamapori kutafuta mbinu za kuwadhibiti tembo kuingia katika makazi ya watu wakifanya uharibifu, hasa katika mashamba karibu na hifadhi.

Mbinu za wataalamu hao zinajumuisha kulima pilipili mashambani, ikitoa matokeo chanya ya kuzuia wanyama kutoharibu mazingira yao.

Hadi sasa imebainika kuwa sahihi kudhibiti tembo kuingia katika maeneo yenye shughuli za binadamu kufanya uharibifu, kutumika njia mbili.

Moja ni kwamba, kunatengezwa tofali la pilipili kwa kutumia kinyesi cha tembo au ng'ombe, kisha kuchanganya na pilipili iliyopondwa au kusagwa na maji.

> **Utakuta mtu kalima ekari yake moja ya mahindi, hapo ndio yanakuwa tayari kwa ajili ya kuvunwa, unaona kundi la tembo linaingia shambani na kuharibu mahindi na wanapoingia, wanaharibu kila kitu hawabakizi kitu hata kimoja.**





Nyingine, ni maarufu ya kutengeneza uzio wa pilipili kwa kutumia 'oili' chafu, vitambaa vya pamba, kamba za katani inayochanganywa na pilipili iliyosagwa kisha kuzungushia shambani kwenye nguzo za miti.

Hizo zinatajwa mkulima anamudu gharama zake, kwani vifaa vingi vinapatikana na mazingira ya shambani na havihitaji pesa nyingi.

Utaalamu kutoka taasisi isiyo ya kiserikali inayoitwa Tembo Pilipili Program (TPP) ya Mikumi, mkoani Morogoro, wanaeleza zamani wakulima walipata shida kukabiliana na tembo wanapoingia katika mashamba yao na kuwaingizia hasara katika mavuno duni au njaa.

Ni kilio kinachotawala tembo wanapoingia shambani na ndipo ikakaribisha hatua ya wakulima kufundishwa namna ya kukabiliana na tembo kwa pilipili, wakitumia gharama nafuu.

Hadi sasa, kuna mradi unaoitwa Tembo Pilipili, ikitumika kwa wakulima wote kijinsia; wake kwa waume kuwakimbiza tembo katika shambani.

Takwimu za Mradi wa Tembo Pilipili, zimefikia wakulima wengi wastani 9,330 katika mikoa kadhaa kwenye vijiji jirani katika hifadhi za: Mikumi, Ruaha, Lake Manyara, Tarangire, Ngorongoro, Bariadi na Hifadhi ya Selous.

Kitaalam inaelezwa, tembo wana uwezo wa kunusa umbali wa zaidi ya kilimeta 20, kutambua mazao.

Awali kabla ya kupata somo la ubunifu huo, wakulima zamani walitumia mbinu zao kuwazuia tembo wasiingie shambani, ikiwamo kuwapigia kelele, madebe au kuchoma moto mipira ya magari kama tairi na viatu.

Pia, mradi huo umekuwa na manufaa ya ama kupunguza au kuondoa ujangili kwa watu wanaowaua tembo kwa faida binafsi," anasema.

**WAKULIMA**

Mkulima kutoka kijiji cha Mhenda, wilayani Kilosa mkoani Morogoro, Blandina Vanali, anasema kabla ya kupata utaalamu huo mpya, walikuwa wanapata changamoto kubwa ya tembo kuingia katika mashamba yao, kukiwapo uharibifu.

"Utakuta mtu kalima ekari yake moja ya mahindi, hapo ndio yanakuwa tayari kwa ajili ya kuvunwa, unaona kundi la tembo linaingia shambani na kuharibu mahindi na wanapoingia, wanaharibu kila kitu hawabakizi kitu hata kimoja," anasema.

Mkulima Blandina anafafanua, kwamba, baada ya kutumia njia za pilipili na 'oili chafu' imewasaidia kwa kiasi kikubwa sasa ni mwaka mmoja, tembo hawajaingia mashambani mwao.

Faida nyingine inatajwa, ni kwa mkulima wa pilipili anaweza kunufaika na kipato cha ziada kwa maana ya bidhaa ya shambani.

Pia, mradi huo wa Tembo Pilipili anautaja kuwasaidia wao wakulima kupata elimu ya kuunda vikundi vya VICOBA, wakiongozwa na maofisa maendeleo ya jamii, wakinufaika na elimu ya utunzaji fedha na kufungua akaunti za benki.

Katika mtazamo huo, ndani yake kuna lengo la kuwawezesha wakulima kujinunulia vifaa vya kutengeneza uzio wa pilipili kukabili tembo shambani, wakajipatia mitaji ya kufanya ujasiriamali.

Mtazamo huo, unagusa kuwawezesha wakulima wanaofuga kuku, mifugo hiyo inapatiwa chanjo hata ufugaji unakuwa wa uhakika zaidi, wakijiongezea kipato.

***• Mwandishi ni mtaalamu wa Mazingira na Mabadiliko ya Tabianchi, mwenye upeo na elimu katika Mradi wa Tembo Pilipili.***

MAZINGIRA

MWENENDO WA DIRA KITAIFA...

# Majaliwa asafiri na ajenda Mazingira ya Rais; Kijaji anuia Azimio Dodoma

• Mkuu wa Nchi anavuka nayo ngazi zote tangu 2010...

**Na Mwandishi Wetu**



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akiwa katika kikao cha mazingira nchini, mwezi huu. **PICHA: MTANDAO**

ANAPOTAJWA kwa wasifu wake Mkuu wa Nchi, Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, amedumu na safari ndefu ya kuwa mdau wa mazingira kitaifa.

Katika Awamu ya Nne ya uongozi, Dk. Samia muda mrefu akidumu Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais, anayewajibika na mazingira.

Ni wajibu alivyovuka nao, wakati fulani Rais wake Jakaya Kikwete, alikuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Mazingira ya Umoja wa Afrika (AU) Mataifa na Waziri Samia, ndiye aliyemsaidia 'kumsukia' majukumu aliyokuwa nayo.

Katika mikono ya kazi yake, Dk. Samia katika jukumu la Mazingira - Ofisi ya Makamu wa Rais, Mkuu wa Nchi, Rais Kikwete akiongoza Kamati ya Mazingira AU, kukawapo ushiriki wa Afrika kuandaa Mkataba wa Paris wa Mazingira, ambao Rais Kikwete amechangia sana.

Hapo kunatajwa nafasi pekee ya Rais Kikwete, akitetea kila mara na rafiki yake aliyekuwa Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa, Ban Ki Moon, kuwezesha nguzo ya Afrika kufanikisha Mkataba wa Paris, mwaka 2015.

Kuna simulizi ya kipekee, Ban Ki Moon, alipomfuata Rais Kikwete katika kikao cha AU jijini Malabo mwaka 2014 akiwa na timu yake kamili - Kamati ya Mazingira AU, wakateta kuwashawishi kufanikisha Mkataba wa Paris uliokuwa shakani, baadhi ya mataifa makubwa wachafuzi wa mazingira yaliposuasua kukubali.

Kuanzia mwishoni mwa 2015, akawa Makamu wa Rais katika Serikali ya Awamu ya Tano chini ya Rais Dk. John Magufuli, mwezi mmoja baadaye, Mkataba wa Paris uliridhiwa baada ya mjalada mzito wa wiki mbili.

Dk. Samia akadumu na jukumu la mazingira ofisini kwake hadi alipokabidhiwa wadhifa wa urais Machi 2021, lakini daima hakuweka mbali ajenda ya mazingira.

Mwaka mmoja na robo baadaye, Rais Dk. Samia akizungumza katika mkutano wa kidini katika Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Julius Nyerere, Dar es Salaam, akasisitiza tena wajibu wa kila mtu kutunza mazingira kwa ushiriki hai.

"Ndugu viongozi wa dini, niwaombe sana kuendelea kushirikiana na serikali kama mnavyofanya sasa katika kuendeleza mapambano ya uharibifu wa mazingira..." akasema Rais Dk. Samia.

Akaeleza magonjwa mengi ya mlipuko hutokea kutokana na uchafu unaotokana na kutotunzwa mazingira, huku akiitaka sekta binafsi kuiga mfano wa viongozi wa dini kuwa mstari wa mbele kwenye juhudi za utunzaji mazingira.

Rais Dk. Samia akatoa wito kwa viongozi katika maeneo yao, kuhakikisha wanasimamia utunzaji mazingira bila kuchoka, huku akiupongeza mkoa Dar es Salaam wakati huo, kushika nafasi ya sita kwa usafi barani Afrika.

### MAJALIWA AENDELEZA

Wiki mbili zilizopita ikiwa miaka miwili na nusu baada ya kauli ya Rais Dk. Samia, inayoonekana kuwa endelevu, Mtendaji Mkuu wa Serikali yake, ambaye ni Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akafafanua:

"Tunapokwenda kuhifadhi mazingira, lazima tuanze na ngazi ya familia na tunapopanda juu tupanue wigo hadi kwa wadau mbalimbali. Viongozi wa dini mnayo nafasi kubwa na hii lazima iwe ajenda maalum, iwe ni ofisi za umma, za binafsi au kwenye taasisi."

Majaliwa alikuwa anafunga mkutano maalum wa viongozi na wadau wa mazingira, uliojadili mwenendo wa mazingira nchini, jijini Dodoma.

Waziri mwenye dhamana ya mazingira nafasi aliyotumikia Dk. Samia kati ya mwaka 2010 na 2015, Dk. Ashati Kijaji, akamsaidia Majaliwa akiufafanua mjumuiko huo wa mwezi huu kwamba una washiriki 2,500 kutoka sehemu mbalimbali, ikiwamo Zanzibar.

"Ninauita huu ni Mkutano Mkuu Maalum (wa Mazingira), kwa sababu umehusisha makundi tofauti ya kijamii wakiwamo viongozi wa dini, wa kisiasa, wa kimila, wanafunzi, wabunge na wadau wengine."

Waziri Mkuu akaendeleza kutafsiri kitendo hicho, ni kuunga mkono juhudi za Rais Dk. Samia, anayeimarisha hifadhi na usimamizi wa mazingira nchini, akimsifu: "Kazi aliyoifanya kwa weledi, ustadi na mafanikio tangu akiwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania."

Majaliwa ambaye kitaaluma ni mwalimu, akafafanua: "Amemudu kusimamia na kutoa miongozo mahsusi ya kuhakikisha mazingira yanahifadhiwa..."

"Leo hii yeye ni Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na tunamwona anaendelea kulisimamia, ili Taifa lifanikiwe katika uhifadhi wa mazingira kwa vizazi vya sasa na baadaye," anasema.

### DHANA MPYA YA RAIS

Waziri Mkuu ametumia fursa hiyo kuwaeleza wajumbe wa mkutano huo, jitihada anazozichukua Rais Dk. Samia kuhakikisha suala la nishati safi linakubalika.

"Rais Dk. Samia Suluhu Hassan amekuja na dhana mpya ya kukataa kukata miti na kutuhamasisha kuhusu nishati safi ya kupikia," anatamka na kuendelea:

"Rais wetu amekuwa kinara wa nishati safi hadi mwezi Mei (2024) alienda Ufaransa kuhutubia kuhusu nishati safi na yeye akiwa ni Mwenyekiti Mwenza wa mkutano huo. Hii ni fahari kwa nchi yetu."

Anasema serikali imetoa fursa kwa wajasiriamali kuanzisha biashara za mitungi na majiko ya gesi kote kitaifa, ili nishati hiyo ipatikane kirahisi, akiwa na msisitizo "huko mbele tutaweka ukomo wa matumizi ya mkaa na kuni."

### KUKABILI CHANGAMOTO

Katika kukabiliana na changamoto za uchafuzi wa mazingira, Waziri Mkuu akasema serikali nchini kihistoria imechukua hatua za kisera na kimkakati kuleta matokeo chanya.

Anazitaja ni kuandaliwa Sera ya Taifa ya Mazingira ya mwaka 2021; Sheria ya Mazingira ya mwaka 2014; kuandaa na kutekeleza Mpango Kabambe wa Taifa wa Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira wa mwaka 2022 hadi 2032.

Mengine ni kuandaa na kutekeleza Mkakati wa Kitaifa wa kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi wa mwaka 2021 hadi 2026; na kutungwa Kanuni na Miongozo inayohusu Masuala ya Mazingira na Mabadiliko ya Tabianchi.

### AIELEKEZA WIZARA

Waziri Mkuu, pia anaitaka wizara inayosimamia mazingira, ishirikiane kwa karibu na wizara za kisekta kuhakikisha maadhimisho ya kitaifa yanayogusa masuala ya mazingira yanatumika kikamilifu.

Anazitaja hatua hizo ni kuiwezesha jamii, kupata uelewa na kuweka alama za kudumu na matokeo yanayopimika kuhusu utunzaji mazingira, ikiwamo Siku ya Upandaji Miti; Siku ya Hali ya Hewa; Siku ya Maji; Siku ya Ardhi Oevu; Siku ya Mazingira; na Siku ya Hifadhi ya Tabaka la Ozoni.

Kuhusu uimarishaji elimu na uhamasishaji kutunza mazingira, Waziri Mkuu ametaka usimamizi sahihi ngazi za mikoa na wilaya, ikiendana na umuhimu wa kuzingatia sheria na kanuni za mazingira, ikibidi itumike mitandao ya kijamii kusambaza elimu hiyo.

"Kuongezeka ufahamu miongoni mwa jamii kuhusu umuhimu wa uhifadhi wa mazingira kutasaidia kupunguza uharibifu na kuimarisha usimamizi wa mazingira.

"Aidha, elimu ijumuishe matumizi endelevu ya rasilimali za mazingira ikiwamo matumizi bora ya ardhi, maji na nishati ili kuhakikisha rasilimali hizo zinabaki kuwa za kudumu kwa vizazi vijavyo," akasisitiza.

### WAZIRI KIJAJI

Waziri wa Nchi (Muungano na Mazingira), Dk. Kijaji, anasema ofisi yake itafuatulia ukamilishaji wa Rasimu ya Azimio la Dodoma kufikia kuwa azimio kamili, kwani linahitaji kufuata utaratibu wa serikali hadi hatua ya kuzinduliwa.

Rasimu iliyowasilishwa mkutanoni na aliyekuwa Katibu Mkuu, Balozi Dk. Bashiru Ali, ikiwa ajenda katika usimamizi na mapitio ya sera na sheria hasa za misitu na uhifadhi; pia uwajibikaji na ushirikishwaji umma, kupitia ugatuzi wa madaraka; usimamizi wa taka ngumu na usafi wa mazingira.

Mengine yakagusa hoja ya upandaji miti, mabadiliko ya tabianchi na biashara ya kaboni; utoaji elimu kuhusu nishati safi; uchumi wa bluu, rasilimali fedha na elimu kwa umma kuhusu mazingira.

# Simulizi ya Mwenyekiti wa Wagumba alivyotaka kuiba mtoto, akashindwa

INATOKAA UK.11

(Mtimblia) kuna dawa unapaka kwenye chuchu za maziwa ya mwanamke.

"Baada ya muda maziwa yanatoka, yaani ningerudi na mtoto ningejikausha kausha hivyo hivyo kwamba sina maziwa ya kutosha, ningetafuta maziwa ya ng'ombe au kopo, kumbe uzao sio wangu. Ila sikufanikiwa!

"Ndio maana pale mwanamke anapoiba mtoto kwenye jamii mimpe adhabu kubwa, wengi wao wameathirika na ugumba, naye anajaribu kufidia ile-'gap' (pengo) la kukosa mtoto," anasema.

Rai yake ni kwamba wanaothubutu kuiba mtoto, hawastahili adhabu kubwa, akitumia uzoefu wake binafsi na majukumu aliyo nayo sasa, anasema anakuwa ameathirika kisakolojia, huku akilalamika taratibu na sheria ya kurithi au kuasili ina mlolongo mrefu.

"Jamii ituamini (kinamama) hata sisi ni walezi wazuri, tena tuna upendo ni wachache wenye ukatili ukifuatilia wameathiriwa na tatizo walilokuwa nalo. Nimelea watoto wa ndugu zangu, lakini mwisho wa siku wanarudi kwao," anasema.

Shamila anasema wagumba wengi wamekata tamaa, hawana wajukuu kwa sababu hawakuzaa na katika baadhi ya jamii, wanaishia kuitwa wachawi.

"Sasa nimeamua tu kuikubali hali yangu na kufanya shughuli zingine kwa sababu suala la uzazi limeshanipita, nimehangaika sana hata," anasema.


Shimila (katikati waliosimama), akiwa na baadhi ya wanachama wa Chama cha Wagumba Tanzania. **PICHA: CHRISTINA MWAKANGALE**

### NAFASI YA TIBA

Mwenyekiti huyo wa Chama cha Wagumba, analalamika licha ya kuwapo kliniki za magonjwa mengi, nafasi hiyo kwa wagumba bado haipo.

Anaendelea: "Hospitalini, tiba za uzazi ziko juu. Tuliuliza huduma za upandikizaji hospitali binafsi ilikuwa karibu shilingi milioni 20. Sawa Muhimbili bei imeshuka kidogo, lakini kuna mtu hata shilingi moja hajawahi kuishika.

"Ummy Mwalimu (Waziri wa Afya) alitupokea, sasa Jenista Mhagama apokee kilio chetu serikali itusaidie, kwamba sisi tutachangia kiasi kidogo.

'Kuna wengine wana ugumba ila hawajapata matibabu sahihi, wakitibiwa watapata watoto..."

Shamila anaeleza kuona faraja baada ya Hospitali ya Taifa Muhimbili kuanzisha kituo maalum cha kuwahudumia, serikali na wadau wengine wa afya, kuwasadia kuchangia gharama za upatikanaji huduma hiyo, takribani Dola za Marekani 5,000 (sawa shilingi 13,611,700), kutokana na wengi wao kuwa na kipato kidogo.

### CHANGAMOTO ZAO

Shamila anasema: "Changamoto zetu nyingi zinafanana, huhitaji wa mtoto. Wengi huduma za afya ya uzazi hawana, pia afya ya akili tatizo wengi wana msongo wa mawazo sababu jamii inatubeza. Kuna wazee ambao hawana watoto nani awatunze, wanashindwa hata mlo mmoja.

"Kubwa ni kwenye ndoa, tumeshaathirika kisaikolojia utakuta umetoka huku ulikoolewa unasema ukipata mwingine, labda utapata mtoto lakini wapi, utashangaa ndani ya mwaka umepitia ndoa mbili au tatu.

"Unaona kila unayempata hayupo sawa, naye mume anakuona huzai, anakuacha. Mimi niliolewa mara mbili, ndoa ya kwanza nimekaa miaka mitatu na ya pili miaka 11.

"Tangu nilipoachwa mwaka 2006 sijaolewa tena. Nimeamua nikae mwenyewe, ingawa nayo si nzuri, inatakiwa uwe na mwenzako, mimi niliachwa nikiwa na miaka 38 bado kijana.

"Ni hivi yaani unaweza ukakaa mwaka 'usishiriki' na mtu yeyote, unaishia tu kutamani...utakaa na ndugu kweli atakusaidia hata ukiumwa, lakini lazima awepo wa ndani yako, akubembeleze, bora niseme hivi kwa sababu nisiposema ndio magonjwa ya akili yanatujaa.

"Tunaumia na mawazo, sonona unaona dunia haina maana. Kwa hiyo, kuanzishwa hiki chama ni kufarijiana. Hata wizi wa mtoto nilijaribu, mwaka 2006 ili nijinusuru.

"Mume wangu alizaa mtoto wa nje. Kijijini usafiri mwingi ni wa baiskeli. Mwanaume anajali sana yule mwanamke aliyezaa nae, wewe hujazaa huna thamani. Kuna siku (mke mwenzie) alimwita kijana aje amchotee maji, sasa ni lazima atumie baiskeli.

"Mume akasema mpe kijana baiskeli akachote maji, nikamwambia baiskeli yangu haitoki na mimi naenda sokoni. Nikamwambie amkodie baiskeli nitalipia, mume hataki ananiambia nina wivu sababu mwenzangu kapata mtoto, kisa nimezuia baiskeli.

'Nilipigwa sana hadi hupoteza fahamu. Mwisho wa siku nikaachwa. Nikaja mjini Dar es Salaam, niseme nina mimba baada ya miezi tisa nirudi na mtoto, lakini miezi tisa ikatimia sioni pa kuiba.

"Ila nafasi yangu ilinisuta kwa azma hiyo. Ila nami nilitaka niheshimike, maziwa ya kunyonyesha sio shida ningepata maziwa ya ng'ombe na kopo ningenunua na kuna dawa unaweka katika matiti ya mama maziwa yangekuja tu. Hata uongee nini katika familia huna maana," anaeleza.

Anasema aliwahi kuonyesha nia ya kuwania uenyekiti wa kijiji au udiwani, ila alikwamishwa na hali yake, kwa madai kwamba 'hana watoto hawezi kuongea...'

### SABABU ZA TATIZO

Shirika la Afya Duniani (WHO), linataja sababu za ugumba ni kwa mtu yeyote anayeshindwa kushika ujauzito kwa kipindi cha mwaka mmoja, licha ya majaribio mengi kufanya hivyo.

Bingwa wa Magonjwa ya Wanawake na Uzazi kutoka MNH, Dk. Living Colman, anasema: "Mzizi wa 'infertility' inategemea na chanzo, kwa mwanamke chanzo kikuu ni 'hormonal imbalance' (mayai kushindwa kupevuka kwa mpangilio) na hii inaweza kutokana na 'genetics' (nasaba), pia ulaji mbaya, sukari nyingi na mafuta, husababisha unene uliopitiliza.

"Pia kupungua sana uzito (anorexia nervosa) inaweza kusababisha ugumba. Mirija kuziba ndio sababu ya pili ya ugumba kwa mwanamke na hii husababishwa na ngono zembe kama nilivyoeleza.

Tabibu Bingwa wa Magonjwa ya Wanawake na Uzazi kutoka Chama cha Madaktari Bingwa wa Wanawake na Uzazi (AGOTA), Dk. Julius Kweyamba, anasema tofauti ya kimaumbile ya mji wa mimba kutokuwa ya kawaida kwa mwanamke, ni miongoni mwa sababu wanawake wagumba na wenye utasa.

"Mama huyu ameumbwa hivyo, mimba zinatoka lakini watu wanakuwa na dhana kwamba huyu hutoa mimba, maumbile hayo ni sababu ya ujauzito kutoka wenyewe.

"Nimeshakutana na baadhi ya kesi (mji wa mimba wenye kasoro) zipo zinazorekebishika na zisizorekebishika," anasema Dk. Kweyamba.

Bingwa huyo ambaye ni Mhadhiri wa Chuo Kikuu cha St. Francis kilichoko Ifakara, Morogoro, anasema pamoja na ishara kuu na dhana iliyojengwa kwenye jamii kwamba mwanamke anayeona siku zake kila mwezi, uwezekano wa kushika ujauzito ni mkubwa, kutokana na kasoro za kimaumbile.

Anasema zipo aina sita za mji wa mimba kwa wanawake na kati ya hizo tano huwa na kasoro, ambazo aidha zinaweza kutibika au kutotibika na kuwa miongoni mwa sababu za ugumba kwa mwanamke.

Bingwa Dk. Living Colman, anaeleza: "Mzizi wa 'infertility' (utasa) inategemea na chanzo. Kwa mwanamke chanzo kikuu ni 'hormonal imbalance' (mayai kushindwa kupevuka kwa mpangilio) na hii inaweza kutokana na 'genetics' (nasaba) lakini pia ulaji mbaya, sukari nyingi na mafuta, husababisha unene uliopitiliza.

"Pia kupungua sana uzito (anorexia nervosa) inaweza kusababisha ugumba. Mirija kuziba ndio sababu ya pili ya ugumba kwa mwanamke na hii husababishwa na ngono zembe kama nilivyoeleza.

"Tiba ya ugumba ni kumuona mtaalamu wa afya (gynaecologist) atafanya vipimo na kugundua tatizo halafu atatoa tiba husika. Kama ni 'hormonal imbalance' atapewa dawa na ushauri. Kama mirija imeziba atashauriwa apandikize (IVF).

Bingwa wa Afya ya Akili kutoka Idara ya Afya ya Akili, Hospitali ya Rufani ya Kanda Mbeya (MZRH), Dk. Raymond Mgeni, anasema kundi hilo hukumbwa na magonjwa ya akili, kutokana na wengine kunyanyapaliwa.

Makamu Mwenyekiti cha Makamu Mwenyekiti wa Chama cha Wataalamu wa Afya ya Akili (MEHATA, Bingwa Mwandamizi wa Afya na Magonjwa ya Akili kutoka Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), Dk. Saidi Kuganda, waliomo kwenye shida hiyo wana maradhi ya msongo wa mawazo na wengine ni sonona.





# Ujenzi kituo cha afya kunufaisha wakazi 11,000

**Na Paul Mabeja,**
MPWAPWA

MFUKO wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) umetoa Sh. milioni 652 kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Afya Lwihomelo kilichoko Kata ya Wangi.

Kukamilika kwa kituo hicho kitahudumia wakazi zaidi ya 11,000 ambao wamekuwa wakitembea umbali mrefu kufuata huduma za matibabu maeneo mengine.

Pia, kitasaidia kupunguza tatizo la vifo vya mama na mtoto ambavyo vimekuwa vikitokea kutokana na watu kujifungulia nyumbani na kukosa huduma za kitabibu kwa wakati.

Akizungumza na waandishi wa habari wakati wa ziara ya viongozi wa TASAF Mkoa wa Dodoma kukagua ujenzi wa kituo hicho, Mratibu wa TASAF Wilaya ya Mpwapwa, Baraka Msuya, alisema fedha za ujenzi wa kituo hicho walizipokea Novemba mwaka jana.

"Fedha za ujenzi wa kituo hicho kwa majengo yote sita tulizipokea kwenye akaunti ya halmashauri Novemba mwaka jana na mradi huu ulipangwa kukamilika ndani ya mwaka mmoja yaani Novemba mwaka huu," alisema na kuongeza:

"Lakini kutokana na changamoto mbalimbali ikiwamo mvua zilikwamisha ujenzi kuanza kwa wakati kutokana na maeneo ulipo mradi wakati wa msimu wa mvua hakupitiki, hivyo baadhi ya vifaa kushindwa kufika eneo la utekelezaji mradi".

Alisema mradi huo unahusisha ujenzi wa jengo la wagonjwa wa nje, nyumba ya watumishi, jengo la kufulia, jengo la mama na mtoto, jengo la upasujai, jengo la kuhifadhia maiti, jengo la maabara pamoja na jengo la kuchomea taka.

**"Kama mwaka jana moja ya changamoto ilikuwa ni mvua pia mwaka huu mvua haiko mbali, hivyo naagiza vifaa vyote viwepo eneo la mradi kabla ya mvua kuanza ili kusiwepo na kisingizio**

Msuya alisema katika utekelezaji wa mradi huo kazi zilizofanyika hadi sasa ni sawa na asilimia 55 na hadi sasa kiasi cha Sh.milioni 386.7 sawa na asilimia 59 ya fedha zote zimetumika na Sh.milioni 265 zimebaki.

Mratibu wa TASAF Mkoa wa Dodoma, Bogit Semhenda, alitoa maagizo matatu ikiwamo kuhakikisha kuwa vifaa vyote vinakuwapo eneo la mradi kabla ya msimu wa mvua kuanza.

"Kama mwaka jana moja ya changamoto ilikuwa ni mvua pia mwaka huu mvua haiko mbali, hivyo naagiza vifaa vyote viwepo eneo la mradi kabla ya mvua kuanza ili kusiwepo na kisingizio kingine tena," alisema.

Kuhusu kusimama kwa ujenzi wa jengo la nyumba ya mtumishi, alimuagiza Mratibu wa TASAF Wilaya kushirikiana na mwanasheria wa halmashauri kuona ni namna gani wanaweza kuvunja mkataba na fundi aliyepewa zabuni bila kuathiri kitu chochote.

Naye Diwani wa Kata ya Wangi, Mdotela Chabruma, aliishukuru TASAF kwa kutoa fedha hizo ambazo zitasaidia wakazi wa eneo lake na kata jirani ya Wotta kupata huduma za kitabibu na kuondokana na tatizo la vifo vya mama na mtoto na kutembea umbali mrefu kufuata matibabu.



Mkuu wa Wilaya ya Dodoma, Jabir Shekimweri (kulia), akikagua maendeleo ya ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Msalato, juzi. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# DC ataka 'speed' ujenzi ukuta Uwanja wa Ndege Msalato

**Na Peter Mkwavila,**
DODOMA

MKUU wa Wilaya ya Dodoma, Alhaji Jabir Shekimweri, ameziagiza kampuni zinazotekeleza mradi wa ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Msalato Mkoani Dodoma kuharakisha kujenga uzio.

Alitoa agizo hilo juzi alipokuwa akizungumza na makandarasi wa kampuni na wafanyakazi wa uwanja huo baada ya kufanya ziara ya ukaguzi.

Amesema kwa kufanya hivyo kutamaliza udokozi wa vifaa unaofanywa na baadhi ya wafanyakazi wasiokuwa waaminifu. Alisema kuwa kuwepo kwa udokozi huo kunaweza kusababisha ucheleweshaji wa uwanja huo ambao umegharimu fedha nyingi na ukashindwa kukamilishwa kwa wakati.

Jabir aliwaagiza makandarasi hao kuharakisha ujenzi wa uzio huo ili kuondoa changamoto hiyo ambayo inaweza kukwamisha makubaliano yaliyowekwa.

Uwanja huo unajengwa na kampuni ya M/s Sinoliydro Corporatian, Beijing Sino - Aero Construction Engineering Co na China Jiangxllut Economie and Techinical Cooperation.

Hata hivyo pamoja na kampuni hizo kuharakishwa ujenzi wa uzio huo pia ameitaka kampuni ya ulinzi ya Suma JKT, Mamlaka ya Wakala wa Barabara (TANROADS) na wananchi wanaoishi karibu na uwanja huo kuhakikisha wanashirikiana na kampuni hizo kuimarisha usalama wa vifaa hivyo. Alisema kuwa uzio huo ukijengwa utaokoa vitu vingi ikiwamo upitishaji wa vifaa vinavyodokolewa na wafanyakazi wasiokuwa na uaminifu pamoja na uchungaji wa mifugo unaofanyika kwa hivi sasa na ukataji wa miti na uchomaji wa mkaa.

Awali akitoa taarifa ya mradi huo, Meneja wa TANROARD Mkoa wa Dodoma, Zuhura Omary, alisema kuwa bado kuna changamoto kwa baadhi ya vibarua pamoja na wafanyakazi kudokoa vifaa mbalimbali vya ujenzi.

Katika taarifa yake alisema kuwa ujenzi wa uwanja huo kuna changamoto ya wizi wa vifaa pamoja na wananchi wanaoishi katika eneo hilo kuchunga mifugo na wengine kukata miti suala ambalo linaloweza kutokamilika kwa wakati kama ilivyokubaliana na serikali.

Zuhura alisema kutokana na changamoto hiyo amewaagiza makandarasi waliopewa mradi wa ujenzi wa uwanja kuhakikisha wanajenga uzio kwa haraka.

# Wakulima milioni nne wajiandikisha kupata mbolea

**Na Renatha Msungu,**
DODOMA

WAKULIMA zaidi ya milioni nne wamejisajili katika mfumo wa upatikanaji mbolea ikiwa ni maandalizi kuelekea msimu ujao wa kilimo.

Aidha, Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA), imewakabidhi vyeti 192 vijana waliopo katika mradi wa BBT waliohitimu mafunzo ya uendeshaji biashara ya mbolea hapa nchini.

Mkurugenzi Mkuu wa TFRA, Joel Laurent alisema hayo jana kwenye hafla ya kukabidhi vyeti kwa vijana hao katika shamba la vijana lililopo Chinangali Chamwino.

Pamoja na mambo mengine alisema vyeti vitawasaidia kujisajili kuwa mawakala wa mbolea ya ruzuku.

Alisema TFRA inaendelea na kampeni ya ushawishi wa matumizi ya mbolea ya ruzuku ikiwamo kutoa elimu ya matumizi sahihi ya mbolea.

"Kwa kutambua umuhimu wa miradi ya kimkakati inayotekelezwa na Wizara ya Kilimo, TFRA imeratibu mafunzo haya kwa kushirikiana na Idara ya Mafunzo ya Wizara ya Kilimo kupitia Vyuo vya Mafunzo ya Kilimo (MATI) ili kutoa mafunzo ya uendeshaji wa biashara ya mbolea kwa kuzingatia Sheria ya Mbolea Na. 9 ya mwaka 2009," alisema.

Alisema matumizi ya mbolea yameongezeka kutoka tani 500,000 kwa mwaka 2022/23 hadi tani 840,000 kwa mwaka 2023/24 ongezeko hilo likichagizwa na ruzuku ya mbolea inayotolewa na serikali.

"Ongezeko la matumizi ya mbolea ni kubwa hii inaashiria namna jamii ilivyoelimika na kutambua umuhimu wa mbolea kwenye shughuli zao za kilimo, TFRA inaendelea kupanua wigo wa utoaji elimu juu ya matumizi sahihi ya mbolea kwa wakulima ili waendelee kunufaika," alisema Laurent.

Hivyo, aliwapongeza vijana wa BBT kutokana na mafunzo waliyopata ambayo yatawajenga katika kilimo wanachoendelea kufanya.

Alisema mafunzo ya siku mbili yaliyotolewa kwao na yana maana kubwa katika maandalizi ya msimu unaoelekea kuanza hivi karibuni.

Pia, aliishukuru Wizara ya Kilimo kutokana na kuwalea vizuri vijana wa BBT jambo linalochangia kuzidi kukua kwa kilimo hapa nchini.

Naye Mratibu wa BBT, Method Kahaya aliishukuru TFRA kwa mafunzo waliyotoa, huku akitoa wito kwamba yasiishie hapo bali yawakumbushe vijana mambo ya kuzingatia kwenye kilimo.



# CWT: Serikali imetatua matatizo yaliyokuwa yanatusibu

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

CHAMA cha Walimu Tanzania (CWT) kimesema serikali imetatua sehemu kubwa ya matatizo yaliyokuwa yanawakabili walimu, hivyo kuwaongezea hali ya kufanya kazi bila ya malalamiko.

Hayo yalielezwa juzi na Rais wa CWT, Leah Ulaya katika mkutano mkuu wa Umoja wa Viongozi CWT Nyanda za Juu Kusini (SOHITCO), uliofanyika mjini Makambako.

Alisema licha ya kutatua matatizo ya walimu lakini serikali imeendelea kuhakikisha Watanzania wanakuwa na uchumi imara kupitia fursa mbalimbali zinazoletwa.

"Nitumie nafasi hii kumshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa namna ambavyo anaendelea kutujali sisi walimu, tunajisemea sisi lakini tunaona ni namna gani anapambana kuhakikisha Tanzania inaendelea kuwa kidedea kwenye uchumi na elimu," alisema Ulaya.

**"Hata kwenye suala la kupanda madaraja Rais Samia ametuona sana sisi walimu, hata mishahara yetu mwalimu mwenye cheti ailingani na kada nyingine," alisema Ambindile.**

Naye Mwenyekiti wa CWT Mkoa wa Njombe, Shabani Ambindile, alisema fedha ya likizo wanaikuta kabla hawajaenda likizo.

"Hata kwenye suala la kupanda madaraja Rais Samia ametuona sana sisi walimu, hata mishahara yetu mwalimu mwenye cheti ailingani na kada nyingine," alisema Ambindile.

Katibu wa chama hicho mkoani Njombe, Felix Mnyanyi alisema moja ya tatizo ambalo linawakabili walimu ni pamoja na baadhi ya wakurugenzi kutowathamini walimu hususani wanapopata ajali kazini, pamoja na kuwapangia kazi za ziada pasipo malipo.

Kwa upande wake, Mkuu wa Wilaya ya Njombe, Kissa Kasongwa akizungumza kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Njombe, Antony Mtaka, aliwataka walimu kuendelea kufanya kazi pamoja na kujishughulisha na shughuli mbalimbali za ujasiriamali, ili kuongeza kipato huku serikaii ikiendelea kutatua matatizo mengine.

"Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini ni mikoa ambayo inaongoza kwa kilimo, mnayo nafasi ya kuwaunganisha walimu na kilimo kwa sababu kilimo ni sehemu ambayo inatoa ajira kubwa sana na fedha nyingi," alisema Kasongwa.

Katibu Tawala Mkoa wa Njombe, Judica Omari aliwataka viongozi wa chama hicho kuendelea kuwahimiza walimu kuhakikisha shuleni kunakuwa mahali salama kwa wanafunzi kupata elimu.





Mkulima, Leocrista Mkope akitoa maoni yake, wakati wa kongamano la kitaifa la siku tatu la wakulima wadogo na mkutano mkuu wa 29 wa Mtandao wa Wakulima Wadogo Tanzania (MVIWATA), lililojumuisha wakulima zaidi ya 1,000 nchini, mjini Morogoro, jana. **PICHA: ZUWENA SHAME**

# CHADEMA Njombe wapata viongozi wapya

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

CHAMA cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) Mkoa wa Njombe kimemchagua Baraka Kivambe kuwa katibu wa chama hicho kwa kipindi cha miaka mitano.

Pia, nafasi ya mwenyekiti wa chama hicho mkoa ikibaki bila kufanyiwa uchaguzi kutokana na kukatiwa rufaa ngazi ya juu.

Hayo yalibainishwa juzi na Katibu wa CHADEMA Mkoa wa Njombe, Baraka Kivambe, baada ya kuchaguliwa kwa kura 35 kati ya 55.

Alisema nafasi ambazo zilifanyiwa uchaguzi ni nafasi ya baraza la vijana, wanawake, wazee na kiongozi wa chama na kufafanua kuwa nafasi ya uenyekiti ikibaki kama ilivyokuwa.

Kivambe alisema kwa utaratibu wa chama chao, Rose Mayemba atabaki kuwa mwenyekiti wa chama hicho hadi pale uchaguzi utakapofanyika upya.

Aidha, katibu huyo alisema kutokana na chama hicho kupata viongozi kwa sasa wamejipanga kuhakikisha wanashiriki kwenye Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, Vijiji na Vitongoji na kueleza kuwa watasimamisha wagombea kila kijiji na mitaa yote.

"Wananchi wote, Watanzania wote wenye sifa ya kuchagua na kuchaguliwa wajitokeze muda utakapofika ili kugombea nafasi katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa," alisema Kivambe.

Naye Katibu wa Baraza la Wazee CHADEMA (BAWACHA) Mkoa wa Njombe, GodLove Mdohe, aliwaahidi wanachama wa chama hicho kufanya kazi kwa bidii ili kufikia malengo yao.

Baadhi ya wanachama wa chama hicho akiwamo Mwenyekiti wa CHADEMA Wilaya ya Njombe, Seth Vegula na Katibu Jimbo la Makambako, Daudi Tweve, walisema nguvu yao kubwa kwa sasa wanaielekeza kwenye Uchaguzi wa Serikali za Mitaa.

Pia walitoa wito kwa wananchi kujiandikisha kwenye Daftari la Makazi ili wapate nafasi ya kushiriki uchaguzi kwa kuchagua viongozi wenye sifa.

# Walioshindwa kulipa bili za maji waondolewa mita

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

MAMLAKA ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Halmashauri ya Mji wa Makambako (MAKUWASA) imeazimia kuwasitishia huduma wananchi ambao wanashindwa kulipia huduma hiyo kwa wakati kwa kuwaondolea mita.

Hayo yalibainishwa juzi na Mkurugenzi wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Makambako, Mhandisi Oscar Lufyagile wakati akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake.

Alisema bado kuna tatizo kwa baadhi ya wananchi kushindwa kulipia huduma ya maji wanayoitumia kwa wakati na kuisababishia mamlaka hiyo hasara.

Mhandisi Lufyagile alisema kutokana na baadhi ya wananchi kushindwa kulipia huduma hiyo, mamlaka itaendesha zoezi la kuwaondolea mita wateja wote ambao wameshindwa kulipia ili wawaunganishie wateja wenye uhitaji na maji.

"Wananchi bado hawajawa na mwamko wa kulima fedha kwa hiyari wakidhani kwamba lile deni linaweza likaenda likajifuta kitu ambacho hakipo," alisema Lufyagile.

Akizungumzia kuhusu mradi wa maji wa Sh. bilioni 42 alisema mradi huo utekelezaji wake umefikia asilimia 25 kwa sasa na kueleza kuwa ukikamilika utatatua tatizo la maji kwa wananchi wa Halmashauri ya Mji wa Makambako.

"Rai yangu wananchi tuwe wavumilivu kwa sababu tumeshavumilia muda mrefu sana ukosefu wa maji, maji machache, maji siyo meupe, sasa kuanzia Oktoba mwakani hapo nukta ndipo itawekwa, wananchi tutakuwa na maji ya kutosha," alisema Mhandisi Lufyagile.

Hata hivyo, Lufyagile alitoa rai kwa wananchi kujiwekea tabia ya kulipia huduma ya maji safi na salama kwa wakati bila kulazimishwa.

Baadhi ya wananchi Makambako, akiwemo Justin Mwangaya alisema hali ya uchumi na bili za maji kutoka kubwa kuliko uhalisia wa matumizi wanayoyatumia ndiyo sababu inayopelekea baadhi yao washindwe kulipia huduma hiyo kwa wakati.

## ‘Kila mwananchi anawajibu kutunza vivutio vya utalii’

Na Rahma Suleiman,
ZANZIBAR

KATIBU Mtendaji wa Kamisheni ya Utalii Zanzibar, Hapsa Mbamba amesema kila mwananchi anawajibu wa kuvitunza vivutio vya utalii kwa sababu utalii ni uti wa mgongo wa uchumi wa Zanzibar.

Alisema hayo juzi wakati akifungua mafunzo ya wajasiriamali na askali wa utalii eneo la Nyamanzi ikiwa ni miongoni mwa shamrashamra za tamasha la fahari ya Zanzibar.

Alisema malengo ya serikali kuona kuwa sekta ya utalii inaendelea kuchukua nafasi kubwa katika uchumi wake na siyo kwa asilimia 30 kama ilivyo sasa.

Mbamba alisema katika kufanya mapinduzi ya kuongeza asilimia hiyo kwa pato la taifa katika uchumi wa Zanzibar wameandaa michezo kwa utalii, mikutano na makongamano ili kuongeza fursa ya watalii wengi kuja kutembelea Zanzibar.

“Tumejipanga katika kuhakikisha tunafanya ubunifu katika kuongeza watalii wanaokuja kutembelea Zanzibar na hivi sasa tumetanua wigo katika michezo kutangaza utalii na mikutano mbalimbali kuja kufanyika Zanzibar,” alisema Mbamba.

Katibu huyo alisema katika kufikia malengo hayo lazima wananchi wawe tayari katika kudumisha amani na utulivu kwa sababu mgeni hawezi kwenda sehemu iliyokuwa na machafuko.

Aidha, alisema kuwa wajasiriamali waliopewa mafunzo hayo wanatakiwa kuwa mabalozi wazuri kwa wenzao ili kutoa huduma zao kwa ukarimu na kuitangaza Zanzibar kupitia bidhaa zao wanazozalisha.

Alisema sekta ya utalii imekuwa ikiajiri vijana wengi kutoka ndani na nje Zanzibar, hivyo wakati umefika kwa vijana hao kuwa wabunifu kwa biashara zao wanazozalisha ili kuendana na soko la kitalii.

Mkufunzi wa mafunzo hayo, Milan Divecha alisema wajasiriamali wananafasi kubwa ya kuutangaza utalii wa Zanzibar lakini lazima wawe wakarimu kwa wageni na kuwa wabunifu katika bidhaa wanazozalisha.

Alisema kuwa siyo vyema kwa wajasiriamali wanapokuwa katika kazi zao kuanza kuiga utamaduni wa mataifa mengine kwasababu Zanzibar inajitosheleza katika utamaduni wake.

# Meli za kigeni 800 zasajiliwa miaka minne

Na Rahma Suleiman,
ZANZIBAR

WIZARA ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi imesema kwa kipindi cha mwaka 2020 -2024 Mamlaka ya Usafiri Baharini Zanzibar (ZMA) imesajili meli 800 kutoka nje zenye uzito wa GT 3,068,376.32, meli za ndani 40 zenye uzito wa GT 58,115.

Naibu Waziri wa Wizara hiyo, Nadil Abdullatif, aliyasema hayo jana katika kikao cha Baraza la Wawakilishi wakati akijibu swali la mwakilishi wa Mtabwe, Dk. Mohamed Ali Suleiman aliyetaka kujua idadi ya meli zilizosajiliwa.

Akijibu swali hilo, alisema kwa kipindi cha 2020- 2024 Mamlaka ya Usafiri Baharini imekusanya Sh. bilioni 10.16 kwa usajili wa meli unaofanywa na ZMA.

“Mheshimiwa Spika, kuhusu mabaharia wazawa kuajiriwa katika meli za kimataifa zinazosajiliwa kupitia ZMA, naomba nilifahamishe kuwa, utaratibu wa uajiri wa mabaharia katika meli ni suala la biashara ya mmiliki wa meli kuchagua mabaharia kutoka nchi yoyote anayotaka,” alisema. Aidha, alisema ZMA inaendelea na mazungumzo ya kuwashawishi wenye meli kuona mabaharia wazawa wenye sifa weweze kuajiriwa katika meli hizo.

**“Mheshimiwa Spika, kuhusu mabaharia wazawa kuajiriwa katika meli za kimataifa zinazosajiliwa kupitia ZMA, naomba nilifahamishe kuwa, utaratibu...**

Alisema mabaharia wazawa wamekuwa wakiajiriwa katika meli za nje kupitia Kampuni ya DANAOS yenye makao makuu yake nchini Ugiriki.

Katika hatua nyingine akijibu swali aliloulizwa kuhusu Zanzibar ina idadi ya mabaharia wangapi wanaofanya kazi katika meli za nje, Nadil alisema kwa sasa Kampuni ya Danaos ina mabaharia 841 ambao wako kwenye meli.

Alisema pia vijana 1,500 wapo wanasubiri kupangiwa kuingia kwenye meli ambao tayari wameshafanyiwa usaili kwa kuajiriwa kupitia kampuni hiyo.

Aidha, alisema serikali inatumia kanuni mbili katika kusimamia fani na ajira za ubaharia nchini kwa mabaharia wazawa, ambazo ni Kanuni ya Maslahi ya Mabaharia 2019 na Kanuni za Uchunguzi wa Afya za Mabaharia 2019.

Alisema pia kutatua migogoro inayojitokeza kati ya mabaharia na wenye meli kuwapatiwa mafunzo na vitendo mabaharia, kufanya vikao vya pamoja kati ya ZMA. Alisema kwa upande wa Chuo cha Ubaharia, serikali tayari imeshaanzisha chuo hicho ambapo kipo chini ya Wizara ya Uchumi wa Bluu na Uvuvi na kinaratibiwa kupitia Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar (SUZA).



Mwakilishi wa Jimbo la Mtambwe, Dk. Mohamed Ali Suleiman, akizungumza wakati akiuliza swali katika kikao cha Baraza la Wawakilishi, Chukwani nje ya mji wa Zanzibar jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Makamu wa Rais ataja malengo Tamasha la Kilimo Hai

Na Mwandishi Wetu

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla, amesema kufanyika kwa Tamasha la Kilimo Hai la Mwaka 2050 ni hatua ya kutimiza malengo ya Dira ya Maendeleo ya Zanzibar ya Mwaka 2050, inayolenga kuwa na maisha bora, endelevu na yenye ustahimilivu kwa wananchi wote.

Alisema hayo jana visiwani hapa katika tamasha hilo lililofanyika katika viwanja vya maonesho ya kilimo Dole Wilaya ya Magharibi “A” Unguja alipomwakilisha Rais Dk. Hussein Mwinyi.

Alisema kufanyika kwa tamasha hilo kunasababisha kuwa na utalii endelevu, kilimo cha asili, ustahimilivu wa hali ya hewa na kufikia malengo ya kitaifa na dhamira ya ulimwengu kwa maendeleo endelevu.

Abdulla alisema dhamira ya kuifanya Zanzibar kuwa kitovu cha utalii endelevu na kilimo hai imeanza kuzaa matunda, kwamba jitihada mbalimbali zinaendelea kuchukuliwa ili kukuza uchumi na kulinda mazingira kwa ajili ya vizazi vya sasa na vijavyo.

Aidha, alisema kilimo hai ni muhimu katika kuhakikisha usalama wa chakula, kuimarisha afya na kulinda mazingira kwa kuiwezesha jamii kupata vyanzo vipya vya maisha pamoja na kuimarisha ustahimilivu wa mifumo ya kilimo dhidi ya mabadiliko ya tabianchi.

Alisema serikali imeweka kipaumbele katika mipango inayounga mkono mbinu mpya za kilimo hai kuanzia kilimo hadi utengenezaji wa bidhaa za kilimo hai zinazoongeza thamani kwenye uchumi wa Zanzibar.

Naye Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo, Shamata Shaame Khamis alisema serikali imejipanga kufanya jitihada kwa kuwashajihisha wakulima na wananchi kufanya kilimo hai chenye kupunguza matumizi ya viatilifu sumu, kulinda mazingira na kuimarisha afya ya mlaji.

Shamata alisema Wizara ya Kilimo itaendelea kushirikiana na wadau kuhakikisha tamasha hilo linaleta tija kwa kuongezeka kwa chakula na kukua kwa uchumi kupitia sekta ya kilimo.

Mwenyekiti wa Kilimo Hai Tanzania, Dk. Mwatima Abdalla Juma, alisema kilimo hai kinazidi kukuwa kwa kasi duniani, kwamba kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo wameandaa mkakati wa kilimo hai Afrika na kutoa nafasi kwa nchi mbalimbali kuja kujifunza Tanzani mbinu na mipango ya kuendeleza kilimo hai.

Dk. Mwatima alisema changamoto kubwa katika kuendeleza kilimo hai nchini inatokana na kuendeleza matumizi ya viuatilifu sumu katika kilimo, ambavyo vinachangia kuongezeka kwa maradhi mbalimbali nchini.

Hivyo, aliiomba serikali kusimamia na kuondoa viuatilifu sumu ili kuendeleza dhana ya kilimo hai.

Aidha, aliitaka serikali kuwapatia ruzuku kwa ajili ya kilimo hai ambayo itatumika kuwasaidia vijana kufanya utafiti utakaoibua mbinu za kuimarisha kilimo hai.

Mkurugenzi kutoka Taasisi ya Kilimo Hai Zanzibar, Ikram Ramadhan Soraga alisema lengo la tamasha la kilimo hai ni kuweka msingi wa maendeleo endelevu pamoja na kukuza uwelewa kwa jamii juu ya kukuza mbinu mpya za kilimo hai Zanzibar.

Alisema tamasha hilo linatoa fursa ya kuwaunganisha pamoja wakulima nchini pamoja na kuwatafutia soko ndani na nje ya nchi kwa lengo la kuimarisha kilimo na kukuza utalii Zanzibar.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA VYETI



**EDSON FRED KIBIKI** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S1144-0080** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **ISIMILA SECONDARY SCHOOL** mwaka 2013 na cheti cha kidato cha sita chenye index namba **S0445-0575** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **MWEMBETOGWA SECONDARY SCHOOL** mwaka 2016. Kwa yeyote atakaeviona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **PHQ/MBE/MBA/29529/2024, PHQ/MBE/MBA/29531/2024**

## KUPOTEA KWA CHETI



**SUDI MOHAMED JUMBE** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba S1071- 0683 kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **ST. MATTHEW'S SECONDARY SCHOOL** mwaka 2016. Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **LUS/PS/B.I/209/**

## KUPOTEA KWA CHETI



**JERRY JOSEPH KISASI** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba S.0692/0095 kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **ROSMINI SECONDARY SCHOOL** mwaka 2021. Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **PHQ/DAR/ILA/206351/2024**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**SELEMANI RASHID MPILI** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **ISUZU TIPPER** yenye usajili namba **T 883 AHR.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA:
**PHQ/DAR/ILA/196 827/2024**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**JULIETH MULUNGI MUTABILWA** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye usajili namba **T 764 DSZ.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA;
**PHQ/LIN/LIN/5002/2024**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**JESSIE WILLIAM MGAYA** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye usajili namba **T 860 DUJ.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
POLISI TAARIFA;
**PHQ/LIN/LIN/4998/2024**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**ELIA MREWA AYO** anatangaza kupotea kwa kadi ya pikipiki aina ya SINORAY yenye usajili namba **MC 243 DQS,** CHASSIS NAMBA: **LD3PCK6J5N2007857** na ENGINE NAMBA: **SR162FMJ22097857.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA:
**PHQ/ARU/MER/35198/2024**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**ARIAS SAID LIAQUAT** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI YENYE USAJILI **T937 CFP** ILIYOPOTEA KWA YEYOTE ATAEFANIKIWA KUIONA KADI HIYO ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI KILICHOPO KARIBU NAE POLISI TAARIFA
**PHQ/IRI/IRI/12013/2024**

## KUPOTEA KWA KADI ZA PIKIPIKI

**METHOD ELIUTER KIWELE** anatangaza kupotea kwa kadi za pikipiki aina ya **FEKON** na **BOXER** zenye usajili namba **MC 323 AEM, MC 548 AVU, MC 104 CZJ, MC 810BZK** na **MC 414 CAG.** Kwa yeyote atakaezipata atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA:
**PHQ/DAR/UBU/183353/2024**

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA**
**WILAYA YA KINONDONI**
**MWANANYAMALA**

**SHAURI LA MADAI NAMBARI.........139 ......LA.....2024**

**SAILAS SARVATORY............MUOMBAJI/WAOMBAJI**

**DHIDI YA**

**1. VENERANDA CHARLES GUGEYE ...MDAIWA/WADAIWA**
**2. BAKARI ISSA LITONGOLELE**

**WITO KUITWA SHAURINI**

**BAKARI ISSA LITONGOLELE**
**POPOTE ULIPO/MLIPO**

**SAILAS SARVATORY** Amefungua /wamefungua shauri mbele ya Baraza la Ardhi na Nyumba lililopo Kinondoni ( Mwananyamala). Shauri husika asubuhi mbele ya **Mh. R. MBILINYI** Hivyo unaamriwa kuhudhuria mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa.

Imetolewa na kutiwa Saini na Mhuri wa Baraza hili leo tarehe 24 Mwezi ...09 ... 2024

MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W) KINONDONI

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA HAKIMU MKAZI KIVUKONI/ KINONDONI**

**MISCELLNEOUS CIVIL APPLICATION No. 20522 YA 2024**

**(Origination from Execution No. 000016034 of 2024)**

**BETWEEN**

**THE REGISTERED TRUSTEES OF MASJID RIDHIWAA...............................................APPLICANT**

**BAINA YA**

**MKITASWIDU IBRAHIM SAID..............1ST RESPONDENT**
**HUFIDHA MKITASWIDU IBRAHIM ( A MINOR) S/T MITASWIDU IBRAHIM SAID, HIS NEXT FRIEND......2ND RESPONDENT**
**REGISTERED TRUSTEES OF RIDWAA ISLAMIC SEMINARY......3RD RESPONDENT**

**Kwa:**
**MKITASWIDU IBRAHIM SAID,**
**HUFIDHA MKITASWIDU IBRAHIM ( A MINOR) S/T**
**MITASWIDU IBRAHIM SAID, HIS NEXT FRIEND,**
**REGISTERED TRUSTEES OF RIDWAA ISLAMIC SEMINARY,**
**DAR ES SALAAM.**

Kwa kuwa mwombaji ameleta maombi ambayo maelekezo ya maombi yameelezwa katika nakala za maombi ambazo zinaweza kupatikana katika mahakama hii, kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria katika mahakama hii ya Hakimu Mkazi Kinondoni/ Kivukoni binafsi au wakili au mwakilishi ambaye anayeruhusiwa kabla au siku ya tarehe 09/10/2024 saaTATU (3:00) kamili asubuhi. Kwa kuwa siku hiyo ni kutajwa kwa shauri unatakiwa kuja na vielelezo vyote vinavyohusiana na maombi haya.
Hati hii imetolewa kwa amri yangu na Chapa ya Mahakama leo tarehe 23/09/2024

HAKIMU MKAZI
MAHAKAMA YA KINONDONI

RESIDENT MAGISTRATE
KINONDONI DISTRICT COURT
DAR ES SALAAM

**IN THE COURT OF DISTRICT DELEGATE OF MOROGORO DISTRICT AT MOROGORO**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO.22853 OF 2024**

**IN the Matter of the late:EDSON JACOB MARIKI**

**1. ESTER EZIKIEL KABULULE**
2.............................................

ALL persons claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate(or letter of administration) is made to the above- named pepetitioner.

Objection to the grant should be filed on or before the ...... day of 03|10|2024.

Dated at Morogoro this ..........day of 19|09|2024.

RESIDENT MAGISTRATE
DISTRICT COURT
P.O.Box 660, Morogoro

***Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa***
***Tupigie,***
***0677 020701***

KWA MAHITAJI YA KUTANGAZA SUMMONS, KUPOTEA KWA CHETI, KUPOTEA KWA KADI YA GARI/PIKIPIKI NA USIMAMIZI WA MIRATHI.
TUPIGIE: +255 - 0677 020701 AU TEMBELEA OFISI ZA MATANGAZO
MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042,
DAR ES SALAAM.
E-MAIL: ADVERTISE@GUARDIAN.CO.TZ

**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTRIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.**
**MOB: +255 - 745 700 710. E-mail: advertise@guardian.co.tz,**
**website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## HABARI KIMATAIFA

# Masharikiya Kati yapewa angalizo

**NEW YORK,** Marekani

VIONGOZI mbalimbali wa dunia ambao wamehutubia mkutano wa Hadhara Kuu ya Umoja wa Mataifa (UN) wameutahadharisha ulimwengu kutokana na kuanza kutanuka kwa vita vya Mashariki ya Kati.

> **Dunia haiwezi kwenda kama ilivyo sasa, ambako changamoto za vita vya Mashariki ya Kati, Sudan, Ukraine na maeneo mengine hazipatiwi majibu wala kutatuliwa.**

Mbali na Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa, Antonio Gutteres, Rais wa Marekani, Joe Biden, na Rais wa Uturuki Recep Erdogan, takribani viongozi wote ambao wamekuwa wakizungumza tangu kufunguliwa kwa mkutano huu wa 79 wa hadhara kuu ya UN Septemba 24 wamekuwa wakijielekeza kwenye mzozo huo wa Mashariki ya Kati.

Rais Luiz da Silva, ambaye nchi yake huwa ya kwanza kuzungumza kutokana na utamaduni wa muda mrefu wa UN, aliyakosowa mashambulizi ya Israel kwenye Ukanda wa Gaza na Lebanon, akisema haki ya kujilinda imegeuka kuwa haki ya kisasi ambayo inazuwia kufikiwa makubaliano ya kuachiliwa mateka na kusitisha mapigano.

Kiongozi wa Qatar, Sheikh Tamin bin Hamad Al-Thani, ambaye nchi yake ni miongoni mwa waongozaji wa mazungumzo ya kusaka amani, aliishutumu moja kwa moja Israel kwa kuwa kizuizi cha mazungumzo ya kusitisha mapigano kwenye Ukanda wa Gaza, akisema kwamba hakuna mshirika wa amani ndani ya serikali ya Benjamin Netanyahu.

Rais wa Baraza la Ulaya, Charles Michel, alisema ingawa Israel ina haki ya kuwepo na kujilinda lakini sio kwa kusababisha mateso kwa raia wanaoishi kwenye maeneo yanayolengwa na jeshi lake.

Naye Rais wa Iran, Masoud Pezeshkian, ambaye nchi yake inaziunga mkono Hizbullah ndani ya Lebabon na Hamas ndani ya Gaza, alilaani kile alichokiita ugoigoi usio maana na usioingia akilini wa UN kwa Israel.

Waziri wa Mambo ya Ndani ya Uingereza, David Lamy, alielezea pia wasiwasi wa nchi yake kwa machafuko yanayoendelea nchini Lebanon, ambayo alisema yanaelekea kuwa vita vikubwa kwenye eneo zima la Mashariki ya Kati.

Ilielezwa kuwa tayari Uingereza imetangaza kuwatuma wanajeshi wake kwenye kisiwa cha Cyprus kusaidia operesheni ya kuwaondoa raia wake kutoka Lebanon.

Mfalme Abdullah wa Pili wa Jordan, alipuuzia uvumi kwamba nchi yake iko tayari kuwapokea Wapalestina wanaolazimika kuyakimbia makaazi yao kutokana na mashambulizi ya Israel, akisema kitendo hicho kitakuwa sawa na uhalifu wa kivita.

Balozi wa Israel kwa UN aliuita mkutano huo wa Umoja wa Mataifa kuwa ni kituko cha mwaka cha unafiki, huku akisisitiza kuwa nchi yake haina haja ya kutuma wanajeshi wake wa ardhini kwenye nchi ya kigeni, akimaanisha Lebanon.

Rais Mahmoud Abbas wa Mamlaka ya Palestina alikikalia kiti chake kwenye ujumbe wa Palestina, ambacho kwa mara ya kwanza kimewekwa kwenye utaratibu wa alfabeti baada ya ujumbe huo kupandishwa hadhi ndani ya Baraza hilo mwezi Mei.

Awali, Katibu Mkuu wa UN, Guterres, aliiambia Hadhara hiyo kuu wakati wa hotuba ya ufunguzi kwamba hali ya uhalifu kutokuchukuliwa hatua, ukosefu wa usawa na uhakika yanaufanya ulimwengu wa sasa kuelekea kwenye mkwamo mkubwa.

Guterres alisema dunia haiwezi kwenda kama ilivyo sasa, ambako changamoto za vita vya Mashariki ya Kati, Sudan, Ukraine na maeneo mengine hazipatiwi majibu wala kutatuliwa. **DW**



Mkutano wa 79 wa Hadhara Kuu ya Umoja wa Mataifa (UN) unaoendelea kufanyika huko New York, Marekani. **PICHA: MTANDAO**

## Rais Sri Lanka avunja Bunge

**COLOMBO,** Sir Lanka

RAIS mpya wa Sri Lanka, Anura Dissanayake, amelivunja bunge la taifa hilo na kuitisha uchaguzi mwingine ikiwa ni ndani ya wiki tatu katika juhudi za kuimarisha mamlaka yake baada ya kupata ushindi kwenye uchaguzi uliofanyika siku chache zilizopita.

Hiyo ni kwa mujibu wa taarifa ya serikali iliyotolewa jana, ambako ilisema kuwa bunge limevunjwa kuanzia Jumanne usiku wa manane, na kwamba uchaguzi wa bunge umepangwa kufanyika Novemba 14, mwaka huu.

Ilielezwa kuwa hatua hiyo ilitarajiwa, kwa kuwa Dissanayake aliapa kufanya hivyo wakati wa kampeni yake ya uchaguzi.

Chama cha Dissanayake kina viti vitatu pekee katika bunge lenye wabunge 225 na uchaguzi wa mapema utamsaidia kudhibiti baraza hilo, huku alama za utendaji kazi wake zikiendelea kuwa imara kufuatia ushindi wake katika uchaguzi wa Jumamosi. **VOA**

# Zimwi la kifo laendelea kumwandama Trump

**WASHINGTON,** Marekani

KAMBI ya kampeni ya rais wa zamani wa Marekani Donald Trump imesema amefahamishwa na idara ya kijasusi ya Marekani kuhusu vitisho kutoka kwa Iran vya kutaka kumuua kiongozi huyo wa upinzani.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na kambi ya kampeni ya Trump, mgombea urais wa Chama cha Republican alifahamishwa kuhusu vitisho vya kweli na mahususi kutoka kwa Iran vya kutaka kumuua katika juhudi za kuyumbisha na kuzusha machafuko nchini Marekani.

Kambi hiyo haikufafanua madai hayo, na haikufahamika mara moja iwapo vitisho iliyokuwa inarejelea ni vipya au viliripotiwa awali.

Ilielezwa kuwa serikali ya Iran haikujibu mara moja ombi la kutaka maoni yake, lakini Tehran hapo awali ilikanusha madai ya kuingilia masuala ya Marekani.

Mkurugenzi wa mawasiliano wa kambi ya kampeni ya Trump, Steven Cheung alisema katika taarifa hiyo kwamba maofisa wa ujasusi wamegundua kuwa mashambulizi yanayoendelea na yaliyoratibiwa yameongezeka katika miezi michache iliyopita.

"Maofisa wa utekelezaji wa sheria katika mashirika yote wanafanya kazi kuhakikisha rais huyo wa zamani Trump analindwa na uchaguzi hauingiliwi," alisema.

Vyombo vya habari vya Marekani viliripoti kwamba maofisa walipokea taarifa za kijasusi kuhusu njama zinazodaiwa kuwa za Iran dhidi ya rais huyo wa zamani. Huku Iran ikikanusha madai hayo na kusema ni ya uovu.

"Iwapo watamuua Rais Trump, jambo ambalo linawezekana, ninatumai kuwa Marekani itaiangamiza Iran, kuifuta kabisa kwenye uso wa dunia, ikiwa hilo halitafanyika, viongozi wa Marekani watachukuliwa kuwa waoga wasio na ujasiri," Trump aliandika kwenye jukwaa lake la Truth Social platform. **BBC**

# KIPA PRISONS AONGOZA ‘CLEAN SHEETS’ LIGI KUU

**Na Mwandishi Wetu**

GOLIKIPA wa Prisons, Mussa Mbisa, anaongoza kwa kucheza mechi nyingi bila kuruhusu goli kwenye nyavu zake.

**Kipa huyo amesimama langoni mara zote ambazo timu yake imecheza mechi nne za Ligi Kuu na hajaruhusu bao lolote.**

Mbisa, kipa wa zamani wa Mwadui na Coastal Union, alisimama langoni Agosti 16, timu yake ikicheza dhidi ya Pamba Jiji, Uwanja wa CCM Kirumba, Mwanza, zikatoka suluhu na suluhu nyingine ilipatikana Agosti 23, Uwanja wa Lake Tanganyika, Kigoma, dhidi ya Mashujaa FC.

Septemba 14, aliiwezesha timu yake kupata suluhu nyingine dhidi ya Tabora United, Uwanja wa Ali Hassan Mwinyi, Tabora, kabla ya kupata ‘clean sheet’ nyingine, Septemba 21, Prisons ikiwa nyumbani dhidi ya Dodoma Jiji na kutoka suluhu.

Kwa mujibu wa takwimu zilizotolewa jana kutoka Bodi ya Ligi, jumla ya makipa wanne wa Ligi Kuu wana ‘clean sheets’ tatu kila mmoja.

Makipa hao ni Denis Donis wa JKT Tanzania, Zuberi Foba



wa Azam FC, Yona Amosi wa Pamba Jiji na Patrick Munthali wa Mashujaa FC.

Takwimu zinasema jumla ya penalti nane zimetolewa kabla ya mechi za jana na tano zilitinga wavuni.

Wafungaji wa mikwaju ya penalti ni Djuma Shaaban wa Namungo aliyefunga katika mchezo dhidi ya Tabora United timu yake ikichapwa mabao 2-1, Heritier Makambo wa Tabora United katika mechi dhidi ya Namungo timu yake ikishinda mabao 2-1, Ibrahim Elias wa KMC katika mchezo dhidi ya Coastal Union ulioisha kwa sare ya bao 1-1, Shedrack Asiegbu wa Tabora United katika mchezo ambao timu hiyo ilishinda bao 1-0 dhidi ya Kagera Sugar na Salum Kihimbwa wa Fountain Gate, akichangia ushindi wa mabao 3-1 dhidi ya Tabora United.

## KMKM ubingwa Ligi Zanzibar lazima

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

KLABU ya KMKM imesema mipango yao mikubwa msimu huu ni kunyakua ubingwa wa Ligi Kuu ya Zanzibar na kupata nafasi ya kushiriki mashindano ya kimataifa.

Kauli hiyo imekuja baada ya juzi kuibuka na ushindi wa mabao 4-1 katika mwendelezo wa michezo ya Ligi kwa kuifunga Zimamoto SC.

Akizungumza na gazeti hili, Kocha Mkuu wa timu hiyo Ame Msimu, alisema kiu yao kubwa ni kuhakikisha wanafanikiwa lengo lao la mbio za ubingwa mwisho wa msimu.

Alisema katika kuhakikisha hilo linafanikiwa benchi lake la ufundi limekuwa makini katika kila mchezo ili mapungufu yanayoonekana uwanjani yafanyiwe kazi mazoezi.

“Ingawa bado mapema kutangaza nia yetu hii, lakini tunataka ijulikane wazi kwa mashabiki wetu, msimu huu lengo letu ubingwa na kushiriki mashindano ya CAF,” alisema Msimu.

Aidha akizungumzia mchezo wao dhidi ya Zimamoto SC alisema licha ya kupata ushindi mnono lakini haukuwa mchezo rahisi.

Alisema wapinzani wao waliwatangulia mbele kwa goli hadi mapumziko, lakini wachezaji wake hawakukata tamaa na kipindi cha pili walipamba na kufanikiwa kupata ushindi huo wa bao 4-1.

“Tunawajua vizuri wapinzani wetu ni miongoni mwa timu nzuri katika soka la Zanzibar, kipindi cha kwanza walikuwa bora lakini kipindi cha pili tulibadilika na kuwazidi kiuchezaji na kupata ushindi,” alisema Msimu.

KMKM SC mpaka sasa imefikisha pointi sita katika michezo mitatu waliyocheza, wameshinda michezo miwili na kupoteza mchezo mmoja, timu hiyo inashika nafasi ya tatu kwenye msimamo wa ligi hiyo yenye timu 16.




Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, Exaud Kigahe (katikati), akicheza ngoma na kikundi cha Hisia cha Temeke wakati wa Maonesho ya Kimataifa ya Vifaa vya Nishati ‘Expo 2024’ katika ukumbi wa Diamond Jubilee, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# *Mghana apewa mikoba ya Mgunda Simba Queens*

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Simba imemtangaza, Yussif Basingi kuwa Kocha Mkuu wa Timu ya Soka Wanawake, Simba Queens, akichukua nafasi ya Juma Mgunda ambaye amemaliza mkataba wake hivi karibuni.

Kocha huyo raia wa Ghana, alitangazwa jana na tayari yupo hapa nchini kukisuka kikosi hicho kinachojiandaa na michezo ya Ngao ya Jamii ambapo Oktoba 2 inatarajia kucheza na Ceasiaa Queens, kabla ya kuanza kwa Ligi Kuu ya Wanawake msimu huu.

Taarifa iliyotolewa na klabu hiyo inaeleza kocha huyo ataanza kuonekana kwenye benchi Oktoba 2 katika mchezo huo utakaochezwa, Uwanja wa KMC Complex, Mwenge, Dar es Salaam.

“Timu yetu ya Simba Queens kuanzia sasa itakuwa chini ya Kocha Mkuu, Basigi ambaye anachukua nafasi iliyoachwa na Juma Mgunda aliyemaliza mkataba wake.

Basigi raia wa Ghana mwenye umri wa maiaka 52 tayari yupo nchini akiendelea kukisuka kikosi cha Queens na anatarajia kuanza kuonekana katika mchezo wa nusu fainali ya Ngao ya Jamii,” ilisema sehemu ya taarifa hiyo.

Kocha huyo anajiunga na Simba Queens akitokea klabu ya Hasaacas Ladies ya nchini kwao Ghana, ambapo mwaka 2015 alipata medali ya dhahabu akiwa kocha Mkuu wa timu ya Taifa ya Wanawake ya Ghana, Black Queens, ambayo aliiongoza kwenye michuano ya All African Games.

Mwaka 2021, aliiwezesha Hasaacas Ladies kumaliza nafasi ya tatu kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika kwa upande wa Wanawake.

Hata hivyo, klabu hiyo imesema kocha Mgosi ataendelea kubaki kuwa msaidizi wa timu hiyo kama ilivyokuwa wakati wa Mgunda.

Mgunda ambaye amezifundisha timu zote za wanaume na wanawake, hakuongezewa mkataba mara baada ya kumalizika, kutokana na kushindwa kuiongoza vyema Simba Queens kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Kanda ya CECAFA

HABARI MICHEZO

ZISIKUPITE

## VLAHOVIC ATAKIWA ARSENAL

ARSENAL inapanga kumsajili mshambuliaji wa Serbia, Dusan Vlahovic mwenye umri wa miaka 24, kutoka Juventus msimu ujao wa majira ya joto. ***(Teamtalk)***

## MADRID YAMTAKA SALIBA

REAL Madrid ina nia ya kumnunua William Saliba, lakini Arsenal hawana mpango wa kumuuza beki huyo wa Ufaransa mwenye umri wa miaka 23. ***(FootballTransfers)***

## UNITED YAMFUATILIA HOWE

KLABU ya Manchester United inafuatilia kwa karibu hali ya kocha, Eddie Howe huko Newcastle United huku mustakabali wake katika klabu hiyo ikitiliwa shaka. ***(Football Insider)***

## WILSON AIVUTIA BRENTFORD

KLABU za Brentford na Fulham zinavutiwa na mshambuliaji wa Newcastle United mwenye umri wa miaka 32, Callum Wilson. ***(Sun)***

## MAN CITY YASAKA KIUNGO

KLABU ya Manchester City inataka kumsajili kiungo mkabaji na wameandaa orodha ya wachezaji wanne walioteuliwa akiwamo kiungo wa kati wa Real Sociedad, Martin Zubimendi, 25, Nicolo Barella wa Inter Milan na nyota wa Atalanta na Brazil, Ederson mwenye umri wa miaka 25, na chipukizi wa Crystal Palace, Adam Wharton mwenye miaka 20. ***(Teamtalk)***

## GUEHI KUMRITHI DIJK L'POOL

LIVERPOOL inamuona mlinzi wa Crystal Palace na England, Marc Guehi mwenye umri wa miaka 24, kama mrithi wa muda mrefu wa mlinzi wa Uholanzi, Virgil van Dijk, 33. ***(Football Insider)***

## MUDRYK KUONDOKA CHELSEA

WINGA wa Ukraine, Mykhailo Mudryk mwenye umri wa miaka 23, anatarajiwa kuondoka Chelsea Januari mwakani. ***(Football Insider)***

## WALIMTAKA IVAN TONEY

KLABU ya Manchester United ilifikiria kumnunua mshambuliaji wa England, Ivan Toney katika usajili wa majira ya kiangazi kabla ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28 kuihama Brentford na kwenda Al-Ahli, lakini hakuendana na wasifu uliotakiwa na kocha Erik ten Hag. ***(ESPN)***

## SESKO BADO AWANIWA UTD

MANCHESTER United bado ina nia ya kumsajili mshambuliaji wa Slovenia, Benjamin Sesko mwenye umri wa miaka 21 kutoka RB Leipzig. ***(GiveMeSport)***

## KIMMICH BASI TENA PSG

KLABU ya PSG imesitisha mpango wa kumnunua kiungo wa kati wa Bayern Munich na Timu ya Taifa ya Ujerumani, Joshua Kimmich mwenye umri wa miaka 29, ili kutoa nafasi kwa Liverpool na klabu zingine zinazomtaka. ***(CaughtOffside)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# ARSENAL KUMPUMZISHA DAVID RAYA

**LONDON,** England

DAVID Raya wa Arsenal anatarajiwa kupumzishwa baada ya kupata jeraha kwenye sare dhidi ya Manchester City.

**Kipa huyo wa Hispania ameanza msimu wa 2024/25 kwa kiwango cha ajabu baada ya mchezo mzuri dhidi ya Tottenham Hotspur katika mchezo wa dabi ya London Kaskazini.**

Raya alipamba vichwa vya habari baada ya kuokoa mara mbili katika sare na Atalanta kwenye mchezo wa Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Kisha akawaokoa washikabunduki hao mara kadhaa wakati wa sare ya bao 2-2 Jumapili kwenye Uwanja wa Etihad.

Hata hivyo, katika kipindi cha pili cha pambano lao la kusisimua na City, Raya alilazimika kupata matibabu kutokana na jeraha.

Licha ya kumaliza mchezo huo, lakini anatazamiwa kuachwa nje katika michezo kadhaa inayofuata ya Arsenal.

Ripoti ya Daily Mail imesema Raya bado ana tatizo la goti, na ingawa haiaminiki kuwa mbaya, Arsenal haitajihatarisha na itamweka nje ya timu yao kwa muda na alikosa mchezo wa jana Jumatano wa kombe la Carabao dhidi ya Bolton kwenye Uwanja wa Emirates.

**Ni baada ya kupata jeraha kwenye mchezo dhidi ya Man City na hawataki ku…**

## HABARI MICHEZO



# GUARDIOLA: HATUJAJUA RODRI ATAKUWA NJE MUDA GANI

**MANCHESTER,** England

PEP Guardiola amesema Rodri atakuwa nje "kwa muda mrefu" kwa sababu ya jeraha la goti alilopata dhidi ya Arsenal, lakini kocha huyo wa Manchester City ana matumaini kuwa huenda akawa nje kwa chini ya muda usiotarajiwa.

Kiungo huyo amesafiri hadi Barcelona kufanyiwa vipimo baada ya kulazimishwa kutoka nje katika kipindi cha kwanza kwenye mchezo uliomalizika kwa sare ya 2-2 Jumapili kwenye Uwanja wa Etihad dhidi ya Arsenal.

Anatazamiwa kufanyiwa upasuaji, lakini Guardiola amesema bado uamuzi haujafanywa kuhusu aina gani ya upasuaji anaohitaji.

Vyanzo vimeiambia ESPN kwamba, kwa mujibu wa uamuzi wa mwisho uliochukuliwa na madaktari, Rodri anaweza kuwa nje kwa kati ya miezi mitano mpaka nane.

"Bado hatuna jibu la uhakika," alisema Guardiola katika mkutano na waaandishi wa habari juzi.

"Atakuwa nje kwa muda mrefu. Lakini kuna maoni kwamba itakuwa chini ya tulivyotarajia.

Sasa hivi siwezi kukuambia. Tunasubiri simu za mwisho na aina ya upasuaji anaohitaji na tunajua hivi karibuni."

Kukosekana kwa Rodri kwa muda mrefu ni pigo kubwa kwa City, ambayo inalenga kushinda taji lao la tano mfululizo la Ligi Kuu England. Amekuwa kiungo muhimu wa kikosi cha Guardiola tangu alipowasili kutoka Atletico Madrid mwaka 2019 na aliisaidia Hispania kushinda Ubingwa wa Ulaya msimu wa joto.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28 ni mmoja wa wanaopendekezwa kuwa anaweza kutwaa tuzo ya Ballon d'Or pamoja na winga wa Real Madrid, Vinícius Júnior.

# *Endrick alistahili kadi nyekundu – Kocha*




**MADRID,** Hispania

KOCHA wa Alavés, Luis Garcia Plaza alisema Endrick alipaswa kutolewa nje kwa kadi nyekundu katika ushindi wa mabao 3-2 wa Real Madrid wa kwenye Ligi Kuu Hispania, LaLiga, Jumanne, baada ya nyota huyo kuonekana akimgonga beki Santiago Mouriño kwa goti lake.

Madrid waliongoza 3-0 katika mchezo huo uliopigwa Santiago Bernabeu shukrani kwa mabao ya Lucas Vázquez, Kylian Mbappé na Rodrygo Goes, kabla ya mabao mawili ya Alavés dakika za lala salama ndani ya dakika mbili.

Endrick alioneshwa kadi ya njano kwa tukio na Mouriño, ambalo lilitokea wakati wachezaji hao wawili walipokuwa wakipishana ndani ya eneo la hatari.

"Ni kadi nyekundu," alisema Garcia Plaza ambaye kwa pamoja alionekana kutupiana maneno makali na kocha wa Real Madrid, Carlo Ancelotti.

"Tulipaswa kucheza dakika 10 zilizopita dhidi ya watu 10.

"Ni nyekundu ya wazi, hakuna anayeweza kusema haikuwa hivyo. Ikiwa mwamuzi hakuiona, hiyo ndiyo maana ya VAR. Labda walipata njano nyingi zaidi kuliko inavyopaswa kuwa, lakini kwa Endrick, ni nyekundu."

Ancelotti alisema hakuweza kutoa maoni yake. "Siwezi kutoa maoni yangu, sikuyaona, na sijaona jibu," alisema kocha wa Madrid.

Chanzo cha klabu kiliiambia ESPN kwamba Endrick atazungumziwa kuhusu tukio hilo ili kuepuka kujirudia katika siku zijazo, ingawa walitaja ujana wake na nguvu kama sababu za kupunguza.

# San Siro yapokonywa uwenyeji fainali Uefa

**MILNA,** Italia

SHIRIKISHO la Soka la Ulaya, UEFA, limefungua upya mchakato wa zabuni ya kuandaa fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya mwaka 2027 baada ya kuupokonya Uwanja wa San Siro wa Milan haki ya kuwa mwenyeji.

San Siro, uwanja wa nyumbani wa AC Milan na Inter Milan, ilichezea fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya kwa mara ya mwisho mwaka 2016 wakati Real Madrid ilipoilaza Atlético Madrid kwa mikwaju ya penalti.

UEFA ilitangaza Milan kuwa mwenyeji kwa mwaka 2027 Mei mwaka huu wakati huo huo wakithibitisha Puskás Aréna huko Budapest, Hungary, kama uwanja wa fainali ya Ligi ya Mabingwa 2026. Lakini licha ya kuthibitisha Milan kama uwanja wa 2027, UEFA ilifanya hivyo kwa masharti kwamba Shirikisho la Soka la Italia (FIGC) liliwasilisha taarifa katika mipango ya ukarabati wa mamilioni ya pauni ya San Siro.

Mipango hiyo bado haijafahamika huku Milan na Inter wakifikiria kuhama San Siro, iliyopewa jina rasmi la Giuseppe Meazza, kutokana na vita vinavyoendelea vya kutafuta ufadhili wa ukarabati wa uwanja uliopo.

Ikiwa fedha haziwezi kupatikana, San Siro yenye uwezo wa kuchukua watazamaji 75,817, ambayo ilifunguliwa mwaka wa 1926, inaweza kubomolewa.

Taarifa ya UEFA ilisema, "Kwa vile Manispaa ya Milan haikuweza kuhakikisha kwamba uwanja wa San Siro na mazingira yake hautaathiriwa na kazi za ukarabati katika kipindi cha fainali ya UEFA 2027, iliamuliwa kutoipa Milan na kufungua tena mchakato wa zabuni ili kuteua uwanja unaofaa, na uamuzi unatarajiwa kutolewa Mei au Juni 2025."

Uwanja wa Allianz Arena wa Munich utakuwa mwenyeji wa fainali ya Ligi ya Mabingwa 2025 Mei 31, lakini ni Budapest na Milan pekee waliowasilisha ombi la kuandaa fainali za 2026 na 2027 wakati mchakato wa zabuni ulipofunguliwa Julai 2023.



## U-15 kamili kuchuana Bosnia

Na Somoe Ng'itu

KOCHA Mkuu wa Timu ya Taifa ya Wasichana wa umri chini ya miaka 15 (U-15), Hilda Masanche, amesema kikosi chake kiko tayari kwenda kupambana katika mashindano ya kimataifa ya UEFA yatakayofanyika baadaye mwezi ujao nchini Bosnia, imeelezwa.

Masanche aliliambia gazeti hili jana anaridhishwa na ushindani unaoonyeshwa katika mazoezi ya timu hiyo na anaamini wataenda kwenye mashindano hayo kusaka ubingwa.



Alisema kwa sasa anamalizika kukamilisha mipango ya namna wachezaji wake watakavyokwenda kupambana katika michuano hiyo inayotarajiwa kufanyika kuanzia Oktoba 2, mwaka huu.

"Tumebakiza siku chache kabla ya kuanza kwa mashindano, lakini niseme sisi tuko tayari kwenda kushindana, kinachofanyika sasa ni kumalizia programu za mazoezi ambazo ni kuona namna gani watacheza kule kulingana na aina ya wapinzani tutakaokutana nao," Masanche alisema.

Aliongeza anatarajia wachezaji wake watatumia uzoefu walioupata katika michuano ya U-12 ambayo ilimalizika hivi karibuni huko China na Tanzania kuibuka mabingwa.

"Tunaamini huu ni wakati wa wachezaji wetu kujifunza mambo mbalimbali kupitia michuano hii tunayoshiriki, ni sehemu ya kuwaandaa kuzoea mashindano ya kimataifa wakiwa katika umri mdogo," aliongeza kocha huyo.

# KARIA AANIKA SIRI SIMBA, YANGA KUNG'ARA AFRIKA

Na Adam Fungamwango

RAIS wa Shirikisho la Mpira wa Miguu Nchini (TFF), Wallace Karia, amesema kufanya vyema kwa Simba na Yanga katika mashindano ya kimataifa ya Afrika kunatokana na umoja na ushirikiano 'mkubwa' kati ya serikali, shirikisho hilo na klabu hizo.

Yanga imetinga hatua ya makundi katika mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika wakati Simba imefuzu kucheza hatua hiyo kwenye michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, Karia alisema umoja huo, umefanya Simba na Yanga kujitengenezea ufalme wake kwenye soka Afrika kwa sasa.

**Karia alisema mafanikio hayo hayakuja kama ndoto, bali yamefanyiwa kazi kubwa, na kuishukuru serikali kwa kuwa bega kwa bega kuwaunga mkono katika mchezo wa soka.**

"Watu wote wanaoongoza sasa hivi wamesimama kutaka mafanikio katika taasisi zao wanazoziongoza, ndiyo asili ya mafanikio haya, tuna mahusiano mazuri sana na serikali, pamoja na wadau mbalimbali zikiwamo klabu husika," alisema Karia.

Alisema TFF itaendelea kushirikiana na serikali pamoja na klabu zote nchini kwa ajili ya kuhakikisha soka la Tanzania linasonga mbele na klabu nyingi zaidi ziweze kufanya vyema katika mashindano ya kimataifa.

Karia amesema hayo siku chache tu baada ya Simba na Yanga kutinga hatua ya makundi ya michuano hiyo ya kimataifa inayosimamiwa na Shirikisho la Mpira wa Miguu Afrika (CAF).

Jumamosi iliyopita, Yanga ilisonga mbele kwa kuisukuma nje CBE ya Ethiopia kwa kuwafunga jumla ya mabao 7-0, ikishinda bao 1-0 ugenini, kabla ya kushinda magoli 6-0 katika mechi ya marudiano iliyofanyika kwenye Uwanja wa New Amaan Complex, Zanzibar.

Hii ni mara ya tatu kwa timu hiyo kutinga hatua hiyo, ambapo mara ya kwanza ilikuwa ni 1998, lakini ni mara ya pili mfululizo kufanya hivyo, baada ya msimu uliopita kutinga hatua hiyo na kuishia robo fainali.

Simba ilifanikiwa kutinga hatua ya makundi, Kombe la Shirikisho Afrika kwa kuichapa Al Ahli Tripoli jumla ya mabao 3-1, ikitoa suluhu ugenini kabla ya kushinda idadi hiyo ya mabao, Jumapili iliyopita kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Inakuwa ni mara ya pili kwa Simba kutinga hatua ya makundi, Kombe la Shirikisho, baada ya kufanya hivyo 2021/22, lakini ni mara ya saba kufanya hivyo mara ya saba kwenye michuano yote ya kimataifa tangu mfumo wa makundi uanzishwe 1998.




Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi (kulia), akipokea zawadi ya jezi kutoka kwa beki wa Simba, Shomari Kapombe, maalum kwa ajili ya kumkabidhi mkewe Mama Mariam Mwinyi (hayupo pichani), wakati kikosi cha Wekundu wa Msimbazi kilipotembelea Ikulu ya Zanzibar. **PICHA: IKULU ZANZIBAR**

# Hafidh: Nitairejesha Mtibwa Sugar Ligi Kuu Bara

Na Adam Fungamwango

STRAIKA wa Mtibwa Sugar, aliyefunga mabao yote mawili katika mchezo wa ufunguzi wa Ligi ya Championship dhidi ya Green Warriors, Raizin Hafidh, ametamba huo ni mwanzo, na atafunga mabao mengi zaidi ili kuisaidia timu yake kurejea Ligi Kuu Tanzania Bara msimu ujao.

Akizungumza na gazeti hili jana kutoka Morogoro, straika huyo wa zamani wa Coastal Union, alisema mabao yake mawili yanaashiria mwanzo mzuri katika kusaka ufungaji bora wa ligi hiyo, pamoja na kuifanya Mtibwa Sugar ifikie malengo yake kurejea kule ambako imezoea.

Ijumaa iliyopita, Mtibwa Sugar iliwachapa Maafande wa Green Warriors mabao 2-0 katika mchezo wa ufunguzi wa Ligi ya Champioship, mchezo uliopigwa kwenye Uwanja wa Manungu Complex, Turuani Morogoro, ambapo straika huyo aliyafunga dakika ya 35 na 70, licha ya kuipa ushindi huo, lakini pia mpaka sasa inaongoza kwenye msimamo pamoja na kwamba ndiyo ni mwanzo wa ligi.

"Nashukuru kwa kuanza ligi vizuri, tumeshinda mabao 2-0 katika mchezo wetu wa kwanza, mabao yote nilifunga mimi, namshukuru Mungu kwa hilo, mimi nikiwa mchezaji wa Mtibwa kwa niaba ya mashabiki wa timu hii.

Tumejipanga vizuri sana msimu huu kwa ajili ya kuhakikisha tunarejea Ligi Kuu msimu ujao, tunawataka wajitokeze kwa wingi katika mchezo wetu ili watupe sapoti kwa ajili ya malengo tuliyojiwekea, nina imani msimu ujao tutacheza tena Ligi Kuu," alisema nyota huyo.

Aliongeza anaamini wanahitaji kujituma zaidi katika kila mechi kwa sababu timu zote zinazoshiriki ligi hiyo ndoto yake ni kupata matokeo mazuri na hatimaye kupanda daraja.

"Tumejipanga na tumedhamiria kufanya vizuri katika msimu huu, tunahitaji kurejea kule tulipopazoea, na ili turejee ni lazima tupate ushindi katika kila mechi, hakuna timu ya kuidharau, mechi zote ni ngumu huku," Hafidh aliongeza.

Mtibwa Sugar ilishuka daraja mwishoni kwa msimu uliomalizika, ikikaa Ligi Kuu kwa miaka 19, tangu ilipopanda 1995, na 1999 na 2000 ikatwaa Ubingwa wa Tanzania Bara.

Timu hiyo inatarajiwa kushuka tena dimbani kesho kwenye Uwanja wa Mabatini ulioko Mlandizi, mkoani Pwani kucheza mechi ya raundi ya pili dhidi ya Mabingwa wa Tanzania Bara mwaka 1968, Cosmopolitan ya Dar es Salaam.

# Michezo

Alhamisi Septemba 26, 2024

Nipashe





Arsenal kumpumzisha Raya

UKURASA 21

# YANGA YATAKATA UGENINI MBEYA

Na Adam Fungamwango

## Bao pekee la Bacca lawabeba, JKT Tanzania pia iking'ara...

BAO pekee lililofungwa na mlinzi wa kati, Ibrahim Hamad 'Bacca', limewapa pointi tatu muhimu mabingwa watetezi, Yanga katika mechi ya raundi ya pili ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya wenyeji KenGold FC iliyochezwa kwenye Uwanja wa CCM Sokoine jijini Mbeya jana.

**Mchezaji huyo alipachika bao kwa kichwa dakika ya 12, akiunganisha mpira wa faulo uliopigwa na Stephane Aziz Ki.**

Lilikuwa ni bao la kwanza kufungwa kwa kichwa na timu ya Yanga msimu huu, huku likiwa la 57 katika Ligi Kuu Tanzania Bara.

Bacca alifunga bao hilo dakika mbili baada ya kuiokoa Yanga isifungwe goli kutokana na mpira wa kona ulioonekana kuingia moja kwa moja wavuni kufuatia mpira wa kona uliopigwa na Makenzi Ramadhani dakika ya 10, ulionekana unataka kuingia wavuni, lakini beki huyo akipiga kichwa cha nyuma na kuurudisha uwanjani, kuinusuru timu yake.

Katika mechi ya jana ambayo mashabiki wengi walidhani Yanga ingepata mabao mengi, haikuwa hivyo kutokana na KenGold kuonekana kucheza kwa nidhamu ya hali ya juu, wakikaa nyuma ya mpira kwa dakika 70 na kuanza kushambulia dakika 20 za mwisho, lakini bahati haikuwa yao.

Yanga ndiyo ilianza mpira huo na moja kwa moja nusura ipate bao bila wapinzani wao kugusa, baada ya shuti la Clatous Chama kudakwa na kipa wa KenGold, Castor Mhagama, ambaye jana alikuwa shujaa kwa kuokoa michomo ya hatari kutoka kwa mabingwa hao watetezi.

KenGold ikajibu shambulizi hilo dakika ya kwanza, ambapo ilifika katika lango la Yanga, lakini straika wake Ramadhani Chobwedo alishindwa kuuweka mpira wavuni uliokuwa umetua ndani ya eneo la hatari, badala yake alipiga hewa, kabla ya mabeki kuokoa.



Kiungo wa Yanga, Clatous Chama (kulia), akijiandaa kumtoka mchezaji wa KenGold FC, Mashimo Daudi katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyochezwa kwenye Uwanja wa CCM Sokoine jijini Mbeya jana. Yanga ilishinda bao 1-0. **PICHA: MTANDAO**

Dakika ya pili, Yanga ilihamia tena langoni kwa Yanga na kufanya mashambulizi mawili ya hatari kutoka kwa Chama na Aziz Ki, lakini umahiri wa kipa, Mhagama uliinyima bao.

Clement Mzize alipata nafasi nzuri na kuukwamisha mpira wavuni dakika tano kabla ya kwenda mapumziko baada ya mabeki wa KenGold kujichanganya walipokuwa wakipasiana, lakini akiwa ana kwa ana na Mhagama, alipiga shuti kali lililopanguliwa na kipa huyo na kuwa kosa.

Kipindi cha pili timu zote zilifanya mabadiliko, ambayo kwa kiasi kikubwa yaliisaidia zaidi KenGold na kuanza kuwazoea Yanga, wakiamua kwenda mbele kushambulia.

Kipindi cha pili Yanga ilitoa Mzize, Chama, Maxi Nzengeli, Aziz Ki na nafasi zao kuchukuliwa na Prince Dube, Pacome Zouzoua, Mudathir Yahaya na Kenneth Musonda.

Dakika ya 80, Joshua Ibrahim nusura aipatie KenGold bao baada ya shuti lake kupaa juu, na nafasi nzuri zaidi ilipatikana dakika tano kabla ya mechi kumalizika pale Helbert Lukindo alipounganisha mpira wa krosi ya Joshua, lakini mpira ukagonga nguzo ya chini na kuonekana kama unatinga wavuni, lakini ulirejea uwanjani huku benchi la ufundi la timu hiyo likiwa limeanza kushangilia.

Huu ni ushindi wa pili kwa Yanga, michezo yote ikicheza ugenini, ilianza msimu mpya kwa kuwafunga Kagera Sugar mabao 2-0, mechi iliyochezwa kwenye Uwanja wa Kaitaba, Bukoba, Kagera huku KenGold ikipoteza mchezo wa tano mfululizo.

Yanga sasa imepanda hadi nafasi ya saba katika msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara ikiwa na pointi sita huku KenGold ikibaki chini kwenye mkia.

Wakati huo huo katika mechi iliyochezwa mapema jana mchana, JKT Tanzania imefikisha pointi sita baada ya kuwafunga Coastal Union mabao 2-1.

## Simba, Azam vitani ugenini

Na Faustine Feliciane

BAADA ya kufuzu hatua ya makundi ya mashindano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika kibabe, Simba inatarajia kushuka ugenini kuwakabili Azam FC katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa New Amaan Complex, Zanzibar.

Ligi Kuu ya Tanzania Bara imehamia kwa muda Visiwani Zanzibar baada ya wenyeji wa mchezo huo, Azam FC kuchagua kuutumia uwanja huo uliofanyiwa ukarabati hivi karibuni.

Kocha Mkuu wa Simba, Fadlu Davids, aliliambia gazeti hili hawatarajii mchezo huo kuwa mwepesi kutokana na ubora wa kikosi cha wapinzani wao Azam FC.

"Azam ni timu nzuri, wanawachezaji wenye uwezo mkubwa, nadhani utakuwa mchezo mzuri na wenye upinzani," alisema Fadlu.

Kocha huyo alisema amekiandaa vizuri kikosi chake kuelekea katika mchezo huo utakaochezwa kuanzia saa 2:30 usiku.

"Tumetoka kwenye mchezo mgumu dhidi ya Al Ahly Tripoli, lakini tumefanya maandalizi kwa ajili ya mchezo huu, ni muhimu sana kwetu kupata ushindi ili tuendelee pale tulipoishia katika michezo yetu ya Ligi Kuu," Fadlu alisema.

Naye Kocha Mkuu wa Azam FC, Rashid Taoussi, ambaye atakuwa anakutana na Simba kwa mara ya kwanza tangu ajiunge na timu hiyo alisema amejindaa vizuri kuwakabili Wekundu wa Msimbazi ingawa amekiri anatarajia mchezo utakuwa mgumu.

Taoussi alisema ugumu wa mechi hiyo unatokana na aina ya mpinzani wanayetarajia kukutana naye.

"Yote kwa yote tumejiandaa vizuri, tunataka pointi tatu ingawa mchezo hautakuwa mwepesi, wachezaji wangu wapo tayari kwa ajili ya mchezo huu muhimu," alisema Taoussi.

Kocha huyo ameanza kufundisha Azam FC hivi karibuni akirithi mikoba iliyoachwa na Yousouph Dabo, ambaye aliondolewa kutokana na matokeo yasiyoridhisha.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >